

**HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA
TEKNOLOJIA**

**MHESHIMIWA PROF. JOYCE LAZARO
NDALICHAKO (MB),**

**AKIWASILISHA BUNGENI MAKADIRIO YA
MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA
MWAKA 2017/18**

DODOMA MEI, 2017

YALIYOMO

VIFUPISHO	v
DIRA	vii
DHIMA	vii
MAJUKUMU	vii
UTANGULIZI	1
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA KWA MWAKA 2016/17	6
KAZI ZILIZOTEKELEZWA MWAKA 2016/17	7
USIMAMIZI WA SERA NA SHERIA ZA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA	7
UBORESHAJI WA MIUNDOMBINU KATIKA TAASISI ZA ELIMU	8
ITHIBATI NA UTHIBITI WA ELIMU NA MAFUNZO SHUGHULI ZILIZOFANYWA NA TAASISI NA MASHIRIKA KWA MWAKA 2016/17	17
USIMAMIZI WA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI	32
MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2017/18	75
URATIBU WA TAASISI NA WAKALA ZILIZO CHINI YA WIZARA	79
SHUKRANI	89
MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2017/18	139
KUTOA HOJA	141
VIAMBATISHO	143
	144

VIFUPISHO

ATC	Arusha Technical College
CKD	Chuo Kikuu cha Dar es Salaam
COSTECH	Commission for Science and Technology
DAAD	Deutscher Akademischer Austausch Dienst
DfID	Department for International Development
DIT	Dar es Salaam Institute of Technology
ESMIS	Education Sector Management Information System
EU	European Union
ESPJ	Education and Skills for Productive Jobs
FDC	Folk Development Colleges
GPS	Global Positioning System
IAEA	International Atomic Energy Agency
ICT	Information and Communication Technologies
IUCEA	Inter-University Council for East Africa
KKK	Kusoma, Kuandika na Kuhesabu
LANES	Literacy and Numeracy Education Support
MMES	Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Sekondari
MTUSATE	Mfuko wa Kuendeleza Sayansi na Teknolojia

MUHAS	Muhimbili University of Health and Allied Sciences
MVTTC	Morogoro Vocational Teacher Training College
NACTE	National Council for Technical Education
NECTA	National Examinations Council of Tanzania
NTA	National Technical Award
TANESCO	Tanzania Electric Supply Company
OVC	Orphans and Vulnerable Children
SADC	Southern Africa Development Community
SIDA	Swedish International Development Agency
SLADS	School of Library Archives and Documentation Studies
SWASH	Schools Water Sanitation and Hygiene
TEA	Tanzania Education Authority
TEHAMAT	Teknolojia ya Habari na Mawasiliano
TET	Taasisi ya Elimu Tanzania
UDSM	University of Dar es Salaam
ToTs	Training of Trainers UKIMWI
	Upungufu wa Kinga Mwilini
UNESCO	United Nations Educational Scientific and Cultural Organization
UNICEF	United Nations Children's Fund
VETA	Vocational Education and Training Authority
VVU	Virusi vya Ukimwi

DIRA, DHIMA NA MAJUKUMU YA WIZARA

DIRA: *Kuwa na Mtanzania aliyeelimika na mwenye maarifa, stadi, umahiri, uwezo na mitazamo chanya ili kuweza kuchangia katika kuleta maendeleo ya Taifa.*

DHIMA: *Kuinua ubora wa elimu na mafunzo na kuweka mifumo na taratibu zitakazowezesha kupata idadi kubwa ya Watanzania walioelimika na wanaopenda kujielimisha zaidi ili waweze kuchangia katika kufikia malengo ya maendeleo ya Taifa letu.*

MAJUKUMU

Kwa mujibu wa Hati Idhini iliyotolewa tarehe 22 Aprili, 2016, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatekeleza majukumu yafuatayo:

- i. *Kutunga na Kutekeleza Sera za Elimu, Utafiti, Huduma za Maktaba, Sayansi, Teknolojia, Ubunifu na Uendelezaji wa Mafunzo ya Ufundii;*
- ii. *Kuendeleza Elimumsingi kwa kutoa Ithibati ya Mafunzo ya Ualimu na Maendeleo ya Kitaalamu ya Walimu;*
- iii. *Kusimamia Uendelezaji wa Mafunzo katika Vyuo vya Maendeleo ya*

- Wananchi;*
- iv. *Kusimamia Mfumo wa Tuzo wa Taifa;*
 - v. *Kuainisha Mahitaji ya Nchi katika Ujuzi na Kuuendeleza;*
 - vi. *Kuweka Viwango vya Taaluma ya Ualimu;*
 - vii. *Kusimamia Ithibati na Uthibiti Ubora wa Shule;*
 - viii. *Kusimamia Huduma za Machapisho ya Kielimu;*
 - ix. *Kutegemeza/Kuimarisha Utumiaji wa Sayansi, Uhndisi, Teknolojia na Hisabati;*
 - x. *Kuendeleza Wataalamu wa ndani katika Sayansi, Teknolojia na Ubunifu;*
 - xi. *Kuratibu na kusimamia utafiti na ubunifu katika fani za Sayansi na Teknolojia;*
 - xii. *Uendelezaji wa Rasilimaliwatu na Uongezaji Tija ya Watumishi walio chini ya Wizara; na*
 - xiii. *Kuratibu Shughuli za Idara, Mashirika, Wakala, Programu na Miradi iliyo chini ya Wizara.*

A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2016/17. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka 2017/18.
2. **Mheshimiwa Spika**, Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano huu na kwa namna ya pekee napenda kumshukuru kwa dhati Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kuendelea kuniamini na kunipa fursa ya kulitumikia Taifa letu na kuwatumikia wananchi wenzangu katika nafasi hii. Ninaahidi kuwa nitaendelea kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi na uadilifu wa hali ya juu. Ninamuomba Mwenyezi Mungu aniongoze na kunisimamia katika kazi zangu zote.
3. **Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt.

John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake thabiti na wenyewe mafanikio makubwa kwa maendeleo ya Watanzania. Ninamshukuru sana Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan pamoja na Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb) kwa maelekezo mazuri na miongozo wanayonipa katika kutekeleza kazi zangu za kila siku. Aidha, ninampongeza Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar, Mheshimiwa Dkt. Ally Mohamed Shein kwa kuiongoza vema Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

4. **Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya pekee ninakushukuru na kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuongoza Vikao vya Bunge hili kwa weledi wa hali ya juu.
5. **Mheshimiwa Spika,** Nawapongeza pia Waheshimiwa Wabunge wote walioteuliwa na Mheshimiwa Rais ambao wameungana nasi katika Bunge hili. Wabunge hao ni Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb), Mheshimiwa Salma Rashid Kikwete (Mb), Mheshimiwa Anne Kilango Malecela (Mb), na Mheshimiwa Abdalla Majura Bulembo (Mb). Aidha, nampongeza pia Mheshimiwa Mchungaji

Getrude Rwakatare (Mb) kwa kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi kuingia kwenye Bunge lako Tukufu katika nafasi ya Viti Maalum pamoja na Mheshimiwa Catherine Nyakao Ruge aliyeteuliwa na Chama cha Demokrasia na Maendeleo kujaza nafasi ya Viti Maalum iliyoachwa wazi na Marehemu Mheshimiwa Elly Macha.

6. **Mheshimiwa Spika**, Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Prof. Palamagamba John Aidan Mwaluko Kabudi (Mb) kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Waziri wa Katiba na Sheria. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wote na Naibu Mawaziri kwa kazi kubwa wanayoifanya katika Serikali hii ya awamu ya tano, ya kuleta maendeleo ya kweli kwa Watanzania. Tunaomba Watanzania wote waendelee kutuunga mkono ili nchi yetu iweze kusonga mbele kwa kasi kubwa zaidi.
7. **Mheshimiwa Spika**, Natoa pia pongezi zangu za dhati kwa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Peter Joseph Serukamba (Mb) kwa kuichambua Bajeti ya Wizara yangu. Ushauri ambao umekuwa ukitolewa na Kamati hii umeiwezesha na utaendelea kuiwezesha Wizara yangu kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

8. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/17 Bunge lako Tukufu liliwapoteza wabunge wenzetu; Mheshimiwa Hafidh Ally Tahir (Mb) aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Dimani - CCM na Mheshimiwa Dkt. Elly Marko Macha (Mb) aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum – CHADEMA. Pia, Taifa letu lilimpoteza Mheshimiwa Samwel John Sitta aliyekuwa Spika Mstaafu wa Bunge la Tisa la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa familia zao, marafiki zao na watanzania wote walioguswa na misiba hiyo. Tunamwomba Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema Peponi.
9. **Mheshimiwa Spika**, kwa masikitiko makubwa sana napenda kuungana na watanzania wenzangu katika maombolezo tuliyonayo kutokana na msiba mzito uliolikumba Taifa letu. Vifo vyta wanafunzi 32, walimu 2 na dereva wa shule ya Msingi ya St. Lucky Vicent, viliyotokana na ajali ya gari iliyotokea Mkoani Arusha tarehe 06/05/2017 vimeacha simanzi na majonzi makubwa kwa watanzania wote.
10. **Mheshimiwa Spika**, Msiba huu umewagusa pia majirani na marafiki zetu ndani na nje ya nchi. Kwa namna ya pekee kabisa namshukuru sana Rais wa Kenya Mheshimiwa Uhuru Kenyatta

ambaye alimtuma Waziri wa Elimu wa Kenya, Mheshimiwa Dkt. Fred Okeng'o Matiang'i kushiriki katika mazishi ya watoto wetu wapendwa, walimu na dereva wao. Serikali ilifarijiwa sana kwa ushirikiano walioituonesha na kwa faraja kubwa waliyotupatia katika kipindi hiki kigumu cha majonzi makubwa. Tunasema Asante Sana.

11. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mara nyingine natoa pole sana kwa wazazi/walezi, ndugu, jamaa, marafiki, uongozi shule, walimu, wanafunzi wa St. Lucky Vicent na wote waliopoteza wapendwa wao katika ajali hiyo mbaya. Hakika, Taifa limepoteza vijana ambaao walikuwa wanajizatiti kielimu ili waweze kulitumikia taifa lao kwa weledi. Tunamuomba Mwenyenzi Mungu azilaze roho zao Mahali Pema Peponi. Aidha, tuendelee kuwakumbuka katika sala zetu, majeruhi watatu waliosalimika katika ajali hiyo na kwa kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu awape uponyaji wa haraka ili waweze kuendelea na masomo yao.
12. **Mheshimiwa Spika**, Baada ya maelezo hayo ya utangulizi sasa naomba nitoe taarifa ya utekelezaji wa kazi za Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha 2016/17 na Mpango wa Bajeti ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2017/18.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA 2016/17

13. **Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka 2016/17 ulizingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 - 2020, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano wa 2016/17 – 2020/21, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030 na Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025. Aidha, utekelezaji wa Mpango ulizingatia pia Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014, Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (1996), Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo (2010), Sera ya Taifa ya Baioteknolojia (2010) na Sera ya Taifa ya Teknolojia za Nyuklia (2013), pamoja na ahadi na maagizo ya Viongozi Wakuu wa Serikali.

B.1 Bajeti iliyoidhinishwa Mwaka 2016/17

14. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/17 Bunge lako Tukufu liliidhinisha kiasi cha Shilingi **1,396,929,798,625.00** ambapo Shilingi **499,272,251,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi **897,657,547,625.00** zilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

15. **Mheshimiwa Spika**, Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2017, jumla ya Shilingi **979,785,341,945.18** zilikuwa zimetolewa kati ya fedha zote zilizoidhinishwa kwa

ajili ya Wizara yangu ambapo Shilingi **350,008,368,423.59** ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida, sawa na asilimia **70.1** ya Bajeti iliyoidhinishwa.

16. **Mheshimiwa Spika**, Fedha za Maendeleo zilizotolewa ni Shilingi **629,776,872,521.59**, sawa na asilimia **70.2** ya Bajeti ya Maendeleo. Aidha, fedha zilizotumika hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2017 zilikuwa ni Shilingi **924,821,633,369.42**, sawa na asilimia **94.4** ya fedha zilizotolewa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **345,545773,733.57** zimetumika kwa Matumizi ya kawaida na Shilingi **579,275,859,725.85** zimetumika kwenye Miradi ya Maendeleo.

KAZI ZILIZOTEKELEZWA MWAKA 2016/17

B.2 Usimamizi wa Sera na Sheria za Elimu, Sayansi na Teknolojia

17. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu ina jukumu la kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na Kanuni katika Sekta ya Elimu ili kuhakikisha kuwa elimu katika ngazi zote inatolewa kulingana na Sheria, Kanuni na Miongozo inayokidhi mahitaji na inayolenga ufanisi katika utoaji wa elimu nchini. Katika mwaka wa fedha 2016/17 Wizara yangu imefanya uchambuzi wa mahitaji ya Mfumo

bora wa kisheria utakaowezesha kuwepo kwa usimamizi na uendeshaji fanisi zaidi wa elimu na mafunzo nchini.

18. **Mheshimiwa Spika**, uchambuzi uliofanyika, pamoja na mambo mengine, ulibaini kuwepo kwa Sheria mbalimbali zinazosimamia maeneo mahususi ya kielimu kama vile Elimumsingi na Sekondari, Elimu ya Ualimu, Elimu ya Juu, Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi, Mitihani ya Taifa na Mitaala. Aidha, katika mfumo huo, imependekewza kuwepo kwa Sheria moja kuu ya elimu kwa kuzingatia Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014. Taasisi zilizo chini ya Wizara zitaendelea na utekelezaji wa majukumu chini ya Sheria zao mahususi kwa kuzingatia muktadha wa Sheria kuu.

B.3 **Uboreshaji wa Miundombinu Katika Taasisi za Elimu**

19. **Mheshimiwa Spika**, Serikali ya Awamu ya Tano inatambua umuhimu wa kuwa na Rasilimali watu walioelimika na watakaoweza kuleta chachu ya maendeleo yatakayowezesha nchi yetu kujenga uchumi wa viwanda. Katika mwaka 2016/17 Wizara yangu ilifanya yafuatayo:

Ukarabati wa Shule Kongwe

20. **Mheshimiwa Spika** Wizara yangu imegharimia ukarabati wa Shule za Sekondari Kongwe 25 ambao unafanyika kama ifuatavyo:
- (i) Ukarabati wa Shule 10 za Jangwani, Azania, Kibaha, Kigoma, Tosamaganga, Songea Wasichana, Malangali, Milambo, Minaki, Ihungo na Nangwa unasimamiwa na Wakala wa Majengo Tanzania –TBA;
 - (ii) Shule 9 za Mpwapwa, Musoma Ufundu, Mtwara Ufundu, Ifakara, Kantalamba, Tanga Ufundu, Ifunda Ufundu, Moshi Ufundu na Bwiru Wavulana zinasimamiwa na Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya – MUST; na
 - (iii) Shule 5 za Iyunga, Zanaki, Kibiti, Ndanda na Tambaza zinakarabatiwa chini ya uongozi wa Shule na Kamati ya Shule.

Ujenzi wa Shule ya Sekondari Ihungo

21. **Mheshimiwa Spika**, Mwezi Septemba 2016 Taifa letu lilipata pigo kutokana na tetemeko lililotokea katika mkoa wa Kagera. Tetemeko hilo lisababisha uharibifu wa miundombinu ikiwemo miundombinu ya Elimu. Napenda kulifahamisha Bunge lako

Tukufu kuwa Serikali ya Uingereza kupitia Idara yake ya Kimataifa ya Maendeleo (DfID) iliipatia Serikali yetu kiasi cha £2.23, sawa na takribani shilingi bilioni 6, kwa ajili ya kujenga upya shule ya Sekondari ya Ihungo ambayo majengo yake yaliharibika kabisa kutokana na tetemeko la ardhi. Kazi ya kujenga upya shule hiyo inayofanywa na Wakala wa Majengo Tanzania imefikia hatua ya kuezeka na itakamilika mwezi Agosti 2017.

Ukarabati wa Shule ya Msingi ya Mugeza Mseto

22. **Mheshimiwa Spika**, Shule ya Msingi ya Mugeza Mseto ambayo inachukua wanafunzi wenye mahitaji maalum ni miongoni mwa shule ambazo majengo yake yaliathirika na tetemeko. Napenda kutoa shukrani za dhati kwa UNICEF kwa msaada wa \$318,000 walioutoa wa kufanya ukarabati wa shule hiyo, kujenga mabweni 4, zahanati 1 na Vyoo 2. Kazi inafanyika chini ya usimamizi wa Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba na imefikia hatua ya kupaua. Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru wadau wote walioungana na Serikali katika kurejesha miundombinu ya Elimu.

Ukarabati wa Vyuo vya Ualimu

23. **Mheshimiwa Spika**, Napenda pia kiliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu imegharimia ukarabati wa miundombinu ya madarasa, maabara, vyoo, mabweni, mifumo ya maji taka na maji safi katika Vyuo vya Ualimu kumi (10) vya Tabora, Korogwe, Kleruu, Butimba, Morogoro, Tukuyu, Kasulu, Songea, Mpwapwa na Marangu kwa lengo la kuongeza udahili wa wanachuo wanaosomea masomo ya Sayansi, Hisabati, TEHAMA na Ualimu wa Elimu ya Awali. Kazi iliyofanyika imeondoa changamoto zote za miundombinu katika vyuo hivyo na kufanya mazingira ya kujifunzia kuwa ya kuvutia zaidi.

Ujenzi wa Miundombinu Mipyä katika Vyuo vya Ualimu

24. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/17, Wizara yangu imendelea na ujenzi na ukarabati Vyuo vinne vya Ualimu vya Kitangali, Mpuguso, Ndala na Shinyanga ambao unafadhiliwa na Serikali ya Canada pamoja na mchango wa Serikali. Hatua ya ujenzi iliyofikiwa katika vyuo hivyo ni kama ifuatavyo:

- (i) **Chuo cha Kitangali:** ujenzi wa nyumba 3 za Wakufunzi umekamilika

kwa asilimia 63, nyumba ya Mkuu wa Chuo imekamilika kwa asilimia 54. Ujenzi wa madarasa, maktaba, ukumbi wa miadhara na majengo mawili ya mabweni yenyewe uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 388 unaendelea;

- (ii) **Chuocha Mpuguso:** ujenziwamabweni mawili yenyewe uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 380 umekamilika kwa asilimia 55, Nyumba ya Mwalimu imekamilika kwa asilimia 85. Ujenzi wa maktaba, Maabara, ukumbi wa miadhara, ukumbi wa mkutano na ujenzi wa vyoo unaendelea;
- (iii) **Chuo cha Ndala:** ujenzi wa nyumba 3 za walimu, nyumba ya Mkuu wa Chuo, majengo 2 ya ghorofa yenyewe uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi 380 na ujenzi wa vyoo unaendelea;
- (iv) **Chuo cha Shinyanga:** ujenzi wa jengo la walimu la ghorofa mbili umekamilika kwa asilimia 80. Ujenzi wa majengo 2 ya bweni, ujenzi wa uzio, jengo la mabweni, majengo 2 ya madarasa, ujenzi wa maktaba na ujenzi wa ukumbi wa miadhara unaendelea.

Ujenzi wa Mabweni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

25. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/17, Serikali imewezesha ujenzi wa mabweni mapya 20 katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mabweni hayo yenye uwezo wa kulaza wanafunzi 3,840 yamejengwa na Wakala wa Majengo ya Serikali chini ya usimamizi wa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa. Ujenzi huo ambao umekamilika ndani ya miezi nane, utasaidia kuondoa adha waliyokuwa wanapata wanafunzi wanapopanga mitaani. Idadi ya wanafunzi watakaolala katika Mabweni haya ni kubwa kuliko idadi ya wanafunzi takriban 2,700 wanaolala katika Mabweni yaliyopo ndani ya Chuo tangu kilipoanza mwaka 1964. Mabweni mapya yalizinduliwa tarehe 15/4/2017 na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli.

Ujenzi wa Maktaba ya Kisasa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

26. **Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa Maktaba mpya ya kisasa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam unaendelea na utagharimu Dola za Kimarekani **Milioni 41** sawa na **Shilingi bilioni 86.1** ambazo zinafadhiliwa na Serikali ya China. Ujenzi

huu unatarajiwa kukamilika mwezi Machi 2018. Maktaba hii itakuwa na uwezo wa kutumiwa na wanafunzi 2,500 kwa wakati mmoja na itakuwa na huduma ya vyumba vya kuendesha Semina, Mikutano pamoja na Mihadhara. Maktaba hii itakuwa ni moja kati ya Maktaba kubwa katika Afrika Mashariki na Kati.

Ujenzi wa Hospitali ya Kufundishia ya Mloganzila

27. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/17 Wizara yangu kupitia Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi Shirikishi Muhimbili ilikamilisha Ujenzi wa Hospitali ya Taaluma na Tiba ya Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi, Muhimbili (MUHAS). Hospitali hii imejengwa katika eneo la Mloganzila lenye ukubwa wa ekari 3,800. Hospitali hii ni ya kisasa kwa miundombinu na vifaa tiba vinavyotumia teknolojia ya kisasa. Hivyo itawezesha utoaji wa mafunzo ya kiwango cha hali ya juu kwa wanafunzi wa Uadtktari, Ufamasia na Uuguzi. Lengo la Serikali ni kuwa na wataalamu wabobezi kwenye eneo la Afya na Tiba.

Kituo cha Taifa cha Uratibu wa Hewa ya Ucaa - SUA

28. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/17 Chuo Kikuu cha Sokoine cha

Kilimo, kimekamilisha ujenzi wa jengo la Kituo cha Taifa cha Uratibu wa Hewa ya Ukaa *National Carbon Monitoring Centre*. Jengo hilo lenye ghorofa moja lina ofisi za walimu, vyumba vya mihadhara, vyumba viwili vya semina ambapo chumba kimoja kina uwezo wa kukaa wanafunzi 60 na chumba kingine kina uwezo wa kukaa wanafunzi 72 na ukumbi wa mikutano. Aidha, jengo hili lina vifaa vya kisasa ambavyo vinatumika kwa ajili ya utafiti na kufundishia hivyo kuweka mazingira yenye ubora wa kufanyia tafiti, ufundishaji, na ujifunzaji. Kukamilika kwa ujenzi huu kumeongeza nafasi za kufundishia wanafunzi 464.

Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Viumbe Hai

29. **Mheshimiwa Spika**, Napenda pia kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuwa ujenzi wa Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Mazingira na Viumbe Maji katika Ndaki ya Sayansi ya Tiba ya Wanyama na Binadamu, kupitia programu ya *Training and Research in Aquatic and Environmental Health in Eastern and Southern Africa (TRAHESA)* katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo awamu ya kwanza umekamilika. Kituo hiki ni cha kipekee kabisa katika eneo la Afrika na Maziwa Makuu katika umahiri wa Sayansi ya Tiba kwa viumbe vya majini.

Kituo kinatoa mafunzo yenyewe kiwango cha hali ya juu ambayo hunufaisha wanafunzi kutoka ndani na nje ya nchi.

Ujenzi wa Maabara ya Sayansi - SUA

30. **Mheshimiwa Spika** ujenzi wa Maabara 4 za Kemia, Baiolojia, Makrobaiojia na Mimea kwa ajili ya Kitivo cha Sayansi Kampasi ya Solomon Mahlangu ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo. Ujenzi huu utaongeza nafasi za kufundishia kwa vitendo kwa wanafunzi 400 wa masomo ya Sayansi kwa wakati mmoja na kuongeza ofisi 22 za Wahadhiri.

Ujenzi wa madarasa na miundombinu ya Shule

31. Wizara yangu imeendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kuratibu uboreshaji wa miundombinu kwenye Shule za Msingi na Sekondari. Wizara yangu imeratibu ujenzi wa miundombinu katika Shule 274 (Msingi 142 na Sekondari 132) katika Halmashauri 119 ambapo ujenzi wa jumla ya Madarasa 1,081, Vyoo 2,802, Mabweni 200, Mabwalo 9, Majengo ya Utawala 6, na nyumba za walimu 11 pamoja na uchimbaji wa visima vya maji katika Shule 4 umefanyika. Ujenzi huu ulitumia njia ya *Force Account* kupitia Kamati za Shule ambayo imesaidia kupunguza gharama za ujenzi na kuongeza

ufanisi katika ukamilishaji wa ujenzi.

32. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inatambua umuhimu wa kuwa na vyoo bora, upatikanaji wa maji safi na salama pamoja na utoaji wa Elimu ya Afya na utunzaji wa mazingira shulenii. Katika mwaka 2016/17, Jumla ya Shule 1,116 (Msingi 1,023 na Sekondari 93) zilijengewa miundombinu ya vyoo bora na kusambaziwa maji safi na salama pamoja na kuunda vikundi vya usafi vya wanafunzi ili kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia na kuongeza mahudhurio.
33. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imechapisha jumla ya Miongozo ya Huduma ya Maji, Afya na Usafi wa Mazingira 3500. Miongozo hii imesambazwa kwenye Mikoa ya Katavi, Songwe, Geita, Njombe, na Simiyu. Miongozo hiyo itasaidia kuweka mipango ya muda mfupi na mrefu ya kuondoa tatizo la upungufu wa vyoo na maji shulenii.

B.4 Ithibati na Uthibiti wa Elimu na Mafunzo

34. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inatambua kwamba Elimu Bora ni muhimu na ina nafasi ya pekee katika kufanikisha maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla, ikiwemo kutimiza azma ya Serikali ya Awamu ya Tano ya kujenga uchumi wa viwanda na kufikia uchumi

wa kati ifikapo mwaka 2025. Hivyo, Wizara yangu imeendelea kuboresha na kuimarisha Mfumo wa Ithibati na Uthibiti Ubora wa Elimu. Katika mwaka 2016/17, kazi zilizofanyika ni kama ifuatavyo:

Ithibati ya Shule za Msingi na Sekondari

35. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kusimamia Ithibati ya Shule ambapo Shule 83 zikiwemo shule za Awali na Msingi 71 na Sekondari 12 zilizokidhi vigezo zilipata usajili. Aidha, vibali vyatya ujenzi wa shule 95 zisizo za Serikali vilitolewa, Wamiliki 86 walithibitishwa. Aidha, Wizara ilitoa vibali vyatya kuongeza Tahasusi za masomo ya Sayansi kwa shule 54 za Sekondari zilizotimiza vigezo kati ya shule 79 zilizowasilisha maombi.
36. **Mheshimiwa Spika**, Sheria ya Elimu sura Namba 353 ya Mwaka 1978, na rekebisho lake la mwaka 1995 na 2002 pamoja na kifungu cha 1V sehemu (c) Kipengele 29 (a) kikisomwa pamoja na kipengele cha 28 vinampa mamlaka Kamishna wa Elimu kutoa usajili kwa shule na kuzifungia shule zote ambazo hazijafuata taratibu. Katika Mwaka 2016/17, Wizara yangu ilifunga shule 10 za kutwa kwa kutoa huduma ya elimu bila kusajiliwa. Hivyo napenda kutoa wito kwa wamiliki wote wa shule kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu

kwani Wizara yangu haitasita kuchukua hatua kwa yeote anayekiuka taratibu.

Uthibiti Ubora wa Shule za Msingi, Sekondari na Elimu ya Walimu

37. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inatambua kwamba Uthibiti Ubora wa Shule ni jambo muhimu katika kuimarisha ubora wa elimu na mafunzo yanayotolewa nchini. Hadi kufikia Aprili 2017, Wizara yangu ilikuwa imekagua shule 7,727 zikiwemo shule za Msingi 6,413 na Sekondari 1,314 sawa na asilimia 71.4 ya shule 10,818 zilizolengwa kukaguliwa. Aidha, ushauri ulitolewa kwa Walimu wa masomo ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Walimu Wakuu, Wakuu wa Shule na Wamiliki wa Shule nao walipata ushauri wa namna ya kuongeza ufanisi katika usimamizi na uendeshaji wa Shule.
38. **Mheshimiwa Spika**, ili kuimarisha Mfumo wa Uthibiti Ubora ndani ya Shule, Wakuu wa Shule za Sekondari 22 na Walimu Wakuu wa Shule za Msingi 312 wamepewa elimu kuhusu Uthibiti Ubora wa ndani ya shule, ambapo shule za Msingi na Sekondari 334 za Mfano zimevezeshwa kuunda Kamati za Uthibiti Ubora wa ndani ya shule na kuweza kujitathmini zenyewe, kubaini changamoto na kuweza kuchukua hatua za utatuzi zilizo ndani ya uwezo

wao. Hatua hizo zitasaidia kupunguza changamoto zinazojitokeza kwa wakati.

39. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inaendelea na uandishi wa Kiunzi cha Uthibiti Ubora wa Shule (*Quality Assurance Framework*) pamoja na kuandaa zana za Uthibiti Ubora wa Shule. Mwongozo huo utakamilika Juni 2017 na utasambazwa katika ofisi zote za Uthibiti Ubora wa Shule Kanda na Wilaya pamoja na wadau wote wa Elimu kwa ajili ya utekelezaji. Ni matarajio ya Wizara kuwa kwa kutumia mwongozo huo, uthibiti ubora utafanyika kwa ufanisi zaidi.

Uboreshaji wa Mazingira ya kufundisha na kujifunzia

40. **Mheshimiwa Spika**, Mazingira ya kufundisha na kujifunza yana mchango mkubwa katika kuinua ubora wa elimu katika ngazi zote. Katika mwaka 2016/17, Wizara yangu ilihuisha Mitaala na Mihtasari ya Elimu ya Awali na Elimu ya Msingi Darasa la I – VI ili izingatie umahiri na kuendana na malengo ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014. Aidha, Wizara yangu inatambua kuwa uwepo wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia na umahiri wa walimu ni mambo muhimu katika kuboresha elimu nchini.

Upatikanaji wa Vitabu Shuleni

41. **Mheshimiwa Spika**, ili kuhakikisha upatikanaji wa vitabu shuleni Wizara yangu imechapisha na kusambaza vitabu shuleni kwa ajili ya Elimu ya Msingi na Sekondari. Jumla ya nakala 6,862,800 za vitabu vya Darasa la II (Awamu ya Pili) na nakala 6,818,181 za vitabu vya Darasa III tayari vimekamilika na kupelekwa shuleni. *Vielelezo Na. 1a na 1b* vinaonesha mgawanyo wa vitabu vya Darasa la II na III kwa kila Wilaya.
42. **Mheshimiwa Spika**, Kwa upande wa Sekondari, nakala 1,958,628 za vitabu vya Sekondari Kidato cha I-IV (*Kielelezo Na. 2 – Vitabu vilivyosambazwa kwa Wilaya*) na nakala 151,055 za vitabu kwa shule za sekondari Kidato cha 5 na 6 vimesambazwa shuleni (*Kielelezo Na. 3 Vitabu Vilivyosambazwa kwa Wilaya*).
43. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafanikio ya kusambaza vitabu shuleni, Wizara imebaini kuwa viro baadhi ya vitabu ambavyo vina makosa ya kimaudhui. Uchambuzi wa kina unafanyika kwa vitabu vyote vilivyochapishwa mwaka 2016/17 ili kubaini endapo dosari zilizobainika katika baadhi ya vitabu hazijajitokeza kwenye vitabu vingine.

44. **Mheshimiwa Spika**, Mchakato wa kuchukua hatua za kinidhamu kwa mujibu wa taratibu za utumishi umekwishaanza kwa watumishi ambao vitabu walivyoidhinisha kuwa viko sahihi vimebainika kuwa na makosa. Napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kuwa hatua kali zitachukuliwa dhidi ya wahusika ili kukomesha tabia ya uzembe kwenye kazi muhimu za taifa. Aidha, baada ya uchambuzi kukamilika kwa vitabu vyote vilivyochapwa, Wizara itafanya pia maamuzi kuhusu hatua za kuchukua dhidi ya vitabu ambavyo vitabainika kuwa na dosari.

Vitabu kwa wanafunzi wenyewe mahitaji maalum

45. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inatambua umuhimu wa kuwawezesha wanafunzi wenyewe Mahitaji Maalum ili wasome kwa ufanisi. Wizara ilichapisha pia nakala 12,400 za vitabu vya kiada kwa Darasa la I katika maandishi ya Nukta Nundu na kusambazwa katika Shule za Msingi 63 zenyе Wanafunzi wasioona (*Kielelezo Na. 4*). Vitabu vya Darasa la II na III kwa wanafunzi wasioona vinaendelea kuchapishwa. Vitabu vya masomo ya Fizikia, Kemia na Hisabati kwa Kidato cha I – II vimesambazwa shulenii kama inavyooneshwa katika *Kielelezo Na. 5*.

Kuimarisha Umahiri wa Walimu katika Ufundishaji

46. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/17 Wizara yangu imetoa mafunzo kuhusu Mtaala ulioboreshwa kwa Walimu 32,015 wanaofundisha Darasa la III na IV kutoka mikoa yote 26 ya Tanzania Bara; na Walimu 519 wanaofundisha wanafunzi viziwi na wasioona wa Darasa la I & II. Mafunzo haya yalilenga kuwajengea uwezo walimu katika ufundishaji na ujifunzaji. Walimu walioshiriki katika mafunzo hayo wameonyesha ari kubwa ya kuimarisha ufundishaji katika shule zao. Ni matarajio ya Wizara kuwa ufanisi wa walimu katika ufundishaji utaendelea kuimarika.
47. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imetoa pia mafunzo kwa wawezeshaji wa Kitaifa 260 *Trainers of Trainers* – (ToTs) katika Mikoa 26 kuhusu ufundishaji wa masomo ya Ufundi ambao watatumika kuendesha mafunzo kwa walimu wengine wa masomo ya Ufundi katika ngazi ya Shule za Sekondari. Vilevile Wizara yangu imeandaa Mwongozo wa Mafunzo Kazini kwa walimu wa masomo ya Ufundi wanaofundisha katika Shule za Sekondari.

Ununuzi na Usambazaji wa Vifaa vya Maabara

48. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu

imenunua vifaa vya maabara vyenye thamani ya **Shilingi bilioni 16.9** kwa Shule za Sekondari 1,696 na vimeanza kusambazwa shuleni ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa Masomo ya Sayansi kwa nadharia na vitendo. Vifaa hivyo vitasambazwa kwa kuzingatia idadi ya shule ambapo ujenzi wa maabara umekamilika (*Kielelezo Na. 6.*)

Ushiriki katika mashindano ya insha

49. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendesha mashindano ya uandishi wa Insha kwa wanafunzi wa sekondari 163 kutoka shule 80 na imetunuku zawadi kwa washindi 10 watakaoingia kwenye mashindano ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na washindi 3 watakaoingia kwenye Mashindano ya *Southern Africa Development Community (SADC)*. Lengo la mashindano hayo ni kuwajengea wanafunzi uwezo wa kufikiri, kuandika kwa ubunifu katika mambo mbalimbali.

Madeni ya Walimu yasiyo ya Mishahara na Motisha kwa Halmashauri

50. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kupitia mradi wa Lipa Kulingana na Matokeo imelipa madeni ya walimu yasiyo ya mishahara yenye thamani ya Shilingi **10,505,160,275.00** kwa walimu **22,420**

kuanzia Julai 2016 hadi Aprili 2017.

51. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kuratibu utoaji motisha kwa Halmashauri 179 zilizohakikiwa mwaka 2015/16 ambapo jumla ya **Shilingi bilioni 22,360,574,170.60** zilitolewa kufuatana na viwango vya utekelezaji wa viashiria vya utendaji katika sekta ya elimu. Mgawanyo wa matumizi ya fedha hizo ulikuwa asilimia 35 ya fedha hizi zitumike kwa ajili ya kurekebisha Ikama ya walimu wa Shule za Msingi ndani ya Halmashauri, asilimia 30 ujenzi wa madarasa na matundu ya vyoo, asilimia 25 ukamilishaji wa maabara na madarasa na asilimia 10 kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini. Kiasi cha fedha za motisha kilichotolewa kwa kila Halmashauri kimewekwa kama *Kielelezo Na 7.*

Elimu Nje ya Mfumo Rasmi

52. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeandaa Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Vituo vya Elimu Nje ya Mfumo Rasmi unaoendana na mazingira ya sasa kwa lengo la kutoa elimu kwa watu walioikosa itakayowasaidia kumudu mazingira yao. Vilevile, imeandaa Mwongozo wa ufundishaji wa KKK kwa watoto wanaosoma nje ya Mfumo Rasmi kwa lengo la kuwasaidia

walimu watakaofundisha madarasa ya Elimu Nje ya Mfumo Rasmi kwa lengo la kuwasaidia walimu watakaofundisha madarasa ya Elimu Nje ya Mfumo Rasmi; Pia, ilihamasisha vijana na watu wazima wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu kutoka mikoa ya Iringa na Singida kujiunga katika madarasa ya kisomo.

Mafunzo ya Walimu

53. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inatambua umuhimu wa kuwa na walimu wenye sifa, maarifa na weledi katika kuinua viwango na ubora wa elimu. Katika mwaka 2016/17 Wizara yangu imefanya yafuatayo katika eneo la Mafunzo ya Ualimu:
- (i) imetoa mafunzo kwa Walimu wa Masomo ya Sayansi 1,946 kwa lengo la kuboresha ufundishaji wa masomo haya katika shule za sekondari za umma na kununua kompyuta 290 kwa ajili ya vituo 20 kwa lengo la kuimarisha ufundishaji wa TEHAMA katika shule za sekondari;
 - (ii) imeandaa Kiongozi cha Mwalimu wa Masomo ya Sayansi kwa wanafunzi wasioona na wenye uoni hafifu. Uwepo wa kiongozi hiki utasaidia wanafunzi wasioona wa sekondari kwa mara ya kwanza kuwezeshwa

kusoma masomo ya sayansi.

- (iii) imeendelea kutoa Mafunzo kwa walimu 17,307 katika Vyuo vya Ualimu 35 vya Serikali na Kuratibu Mafunzo kazini kwa wakufunzi 194 wa masomo ya Sayansi na Hisabati kwa kutumia TEHAMA. Lengo ni kuandaa walimu mahiri katika ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya Sayansi na Hisabati kwa kutumia TEHAMA.
- (iv) imeendesha Mafunzo kabilishi kwa wakufunzi 344 wanaofundisha Mtaala wa Stashahada Maalum ya masomo ya Sayansi, Hisabati na TEHAMA katika vyuo 7 vya Ualimu vya Mpwapwa, Butimba, Morogoro, Kasulu, Korogwe, Tukuyu na Songea.
- (v) imeanza kupitia mtaala wa Ualimu ngazi ya Cheti na Stashahada ili kuendana na mtaala wa Elimumsingi ulioboreshwani na pia kuzingatia mahitaji ya sasa.
- (vi) imetoa mafunzo kwa Wakufunzi 22 juu ya uingizwaji wa masuala mtambuka katika ufundishaji. Masuala hayo ni pamoja na: Elimu Jumuishi, Usawa wa Kijinsia, Haki na Usalama wa Mtoto, Afya na

Mazingira Salama ya Shule, Stadi za Maisha, Elimu ya Jinsia na Virusi vyta UKIMWI, na Elimu ya Mazingira.

- (vii) ilitoa mafunzo kwa Wakufunzi 24 kutoka vyuo vya Ualimu Mpuguso, Tandala na Tukuyu juu ya uchopekaji wa stadi za KKK katika masomo ya darasa la III hadi la VI.
- (viii) imenunua na kusambaza vifaa na Kemikali kwa ajili ya maabara za Vyuo vya Ualimu vya Kasulu, Korogwe, Tukuyu, Butimba, Songea, Kleruu, Morogoro, Mpwapwa na Tabora ili kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa vitendo;
- (ix) imenunua vifaa vya TEHAMA zikiwemo Kompyuta 30, Kompyuta Mpakato 2 na Projekta 2 kwa kila chuo kwa vyuo vyote 10 ili kuimarisha ufundishaji wa walimu tarajali wa masomo yote hasa wanaosomea ufundishaji wa somo la TEHAMA.

Kuimarisha Utoaji wa Elimu kwa Wanafunzi wenyewe Mahitaji Maalum

54. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu inatambua umuhimu wa elimu katika kuleta maendeleo ya Taifa na kwamba elimu ni haki ya msingi ya kila Mtanzania.

Hivyo, Wizara yangu imeendelea kutoa fursa ya elimu kwa wanafunzi wenyе Mahitaji Maalum kwa kununua vifaa mbalimbali vya kielimu na visaidizi kwa wanafunzi wenyе baki ya usikivu na wasioona. *Kielelezo Na. 8* kinaonesha vifaa vilivyosambazwa na usambazaji wake kiwilaya.

55. **Mheshimiwa Spika**, Vifaa vilivyonunuliwa vinajumuisha Mashine za kuandikia maandishi ya nukta nundu (Braille) 932; Vivunge (kits) vyenye vifaa vya msingi vya kujifunzia kwa wanafunzi wasioona 1,495; karatasi za kuandikia maandishi ya nukta nundu rimu 2,548; Karatasi za kurudufishia maandishi ya nukta nundu rimu 1,150; na Shime sikio - Hearing Aids kwa ajili ya wanafunzi wenyе baki ya usikivu (hard of hearing) 1,150.
56. **Mheshimiwa Spika**, Vifaa hivi vitawezesha kuongeza fursa za kushiriki kwa ufanisi katika Elimu kwa Wanafunzi wenyе mahitaji maalum. Aidha, Wizara yangu imeendelea kununua vivunge vya upimaji kwa ajili ya kubaini mahitaji ya ujifunzaji kwa watoto wanaoandikishwa shule. Vifaa hivi vimesambazwa katika mikoa yote Tanzania Bara. *Kiambatisho Na. 9* kinaonesha aina ya vivunge na usambazaji wake.

57. **Mheshimiwa Spika**, Ili kuimarisha ufundishaji wa masomo ya Fizikia, Kemia na Hisabati kwa wanafunzi wasioona, Wizara yangu imeandaa Miongozo mitatu ya kufundishia na vitabu ili kuwawezesha Wanafunzi kujifunza masomo hayo kwa ufanisi zaidi. Aidha, nakala 4,400 za vitabu vikiwemo 1,400 vya Fizikia, 1,400 vya Kemia na 1,600 vya Hisabati vimechapishwa kwa maandishi ya Nukta Nundu na kusambazwa katika Shule zote 25 za Sekondari zenye Wanafunzi Wasioona. *Kiambatisho Na. 10* kinaonesha usambazaji wa vitabu hivyo.
58. **Mheshimiwa Spika**, Vifaa hivi vitawezesha kuongeza fursa za kushiriki kwa ufanisi katika Elimu kwa Wanafunzi wenyewe mahitaji maalum. Aidha, Wizara yangu imeendelea kununua vivunge vya upimaji kwa ajili ya kubaini mahitaji ya ujifunzaji kwa watoto wanaoandikishwa shule.
59. **Mheshimiwa Spika**, Ili kuimarisha ufundishaji wa masomo ya Fizikia, Kemia na Hisabati kwa wanafunzi wasioona, Wizara yangu imeandaa Miongozo mitatu ya kufundishia na vitabu ili kuwawezesha Wanafunzi kujifunza masomo hayo kwa ufanisi zaidi. Aidha, vitabu vya Fizikia, Kemia na Hisabati vimechapishwa kwa maandishi ya Nukta Nundu na

kusambazwa katika Shule zote 25 za Sekondari zenye Wanafunzi Wasioona.

Kuimarisha upatikanaji wa Takwimu za Elimu

60. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeimarisha Mfumo wa Upatikanaji na Utoaji wa Takwimu za Elimu (*Education Sector Management Information System - ESMIS*) kwa kutoa mafunzo juu ya matumizi ya mfumo huo kwa Maafisa Elimu Taaluma wa Mikoa yote Tanzania Bara na Maafisa Elimu wa Vifaa na Takwimu wawili kutoka kila Halmashauri. Upatikanaji wa takwimu kwa wakati utawezesha kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera, kuandaa mipango ya elimu na kutoa maamuzi stahiki.

Kuimarisha Sayansi, Teknolojia na Ubunifu.

61. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu ina jukumu la kusimamia na kuendeleza Sayansi, Teknolojia na Ubunifu pamoja na matumizi yake katika kuchochaea maendeleo ya uchumi wa viwanda. Katika mwaka 2016/17, Wizara yangu imeandaa rasimu ya Mwongozo wa Kutambua Wabunifu na Wagunduzi nchini *National Inventions and Innovations Guidelines* kwa lengo la kuendeleza bunifu na gunduzi zao ili kuchochaea maendeleo ya Taifa. Aidha, imefanya mapitio ya Mkataba wa

Makubaliano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Uswisi ili kuimarisha ushirikiano na kupanua wigo wa ushirikiano kwa kuzihusisha taasisi nyingine za Tafiti na kuongeza maeneo ya ushirikiano kwenye nyanja za Sayansi, Teknolojia na Ubunifu.

SHUGHULI ZILIZOFANYWA NA TAASISI NA MASHIRIKA KWA MWAKA 2016/17

62. **Mheshimiwa Spika,** Wizara yangu imeendelea kuratibu kazi za Taasisi, Wakala na Vyuo vya Elimu ya Juu vya Umma. Shughuli zilizofanyika katika mwaka 2016/17 ni kama ifuatavyo:

Taasisi ya Elimu Tanzania

63. **Mheshimiwa Spika,** Taasisi ya Elimu Tanzania inalo jukumu la kuandaa Mitaala na Mihtasari, kutoa Miongozo kuhusu vifaa vya kufundishia na kujifunzia, kutoa Mafunzo kwa Walimu kazini na kufanya utafiti na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mitaala katika Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Ualimu. Katika mwaka 2016/17 Taasisi ya Elimu ilifanya kazi zifuatazo:

- (i) Ilipitia Mtaala na mihtasari ya Elimu ya Awali, Darasa la I –VI kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza na kuandaa Miongozo ya walimu ya

Elimu ya Awali, Darasa la I –VI kwa lugha ya Kiswahili na Kiingereza.

- (ii) ilikamilisha Miswada 18 ya vitabu vyatya Darasa la IV hadi la VI vinavyokidhi mahitaji ya utekelezaji wa mtaala, pamoja na kuandika Vitabu vyatya Kiada aina 22 kwa kuzingatia Mtaala ulioboreshwani.
- (iii) ilisambaza nakala 60,672 za Mtaala, nakala 303,360 za Mihtasari na nakala 1,840,183 za vitabu vyatya kiada Darasa la III – VI.
- (iv) ilifanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mtaala kwa Darasa la I na II katika mikoa 10 ya Tanzania Bara. Mikoa hiyo ni: Dar es Salaam, Mtwara, Lindi, Ruvuma, Tabora, Geita, Dodoma, Singida, Arusha na Mbeya.
- (v) imehuisha Mihtasari ya Masomo ya Mchepuo ya Sayansi Kimu, Ufundi na Kilimo Kidato cha 1 - 4 na kuchapisha Vitabu vyatya kiada aina 30 vyatya Kidato cha 1 - 4 na aina 15 za vitabu kwa Kidato cha 5-6. Aidha, imeandaa Mihtasari 18 ya Sekondari Kidato cha 1-6 inayoendana na Mtaala wa mwaka 2005; na kusambaza nakala 1,531,627 za vitabu vyatya kiada kwa Kidato cha 1 – 6 katika mikoa 20 ya Tanzania Bara.

(vi) imetoa Mafunzo kwa wawezeshaji 22 wa kitaifa kutoka katika Vyuo vya Ualimu, Taasisi ya Elimu Tanzania (TET), Agha Khan Foundation, Right to Play na Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule, wakufunzi 375 na walimu 16,129 wa Elimu ya Awali katika vituo 19 Tanzania Bara; na mafunzo kwa Wakuu wa Vyuo 22 kutoka Vyuo vya Serikali na watatu (3) kutoka Vyuo Visivyo vya Serikali vinavyotoa mafunzo ya Elimu ya Awali kuhusu uendeshaji wa mafunzo ya Walimu wa Elimu ya Awali.

Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi Stadi (VETA)

64. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi Stadi (VETA) ina majukumu ya kuratibu, kuthibiti, kugharimia, kutoa na kukuza Mafunzo ya Ufundsi Stadi nchini. Katika Mwaka 2016/17, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundsi Stadi (VETA) ilitekeleza kazi zifuatazo:

(i) Ilidahili Wanafunzi 11,672 wa Mafunzo ya Ufundsi Stadi ya muda mrefu katika Vyuo 28 vya Ufundsi Stadi vya VETA wakiwemo Wanawake 3,286 na Wanaume 8,386 ikilinganishwa na lengo la udahili wa

wanafunzi 10,463.

- (ii) Ili kuongeza fursa za kujiunga na Mafunzo ya Ufundı Stadi, iliendelea na ujenzi wa Vyuo vya Ufundı Stadi kama ifuatavyo:-
- (a) Ujenzi wa Chuo cha Ufundı Stadi cha Njombe Wilayani Ludewa umeanza katika ngazi ya uchimbaji msingi.
 - (b) Ujenzi wa Chuo cha Ufundı Stadi Namtumbo ambao upo katika hatua ya ujenzi wa misingi ya majengo mbalimbali.
 - (c) Ujenzi wa Jengo la Utawala katika Chuo cha Ufundı Stadi Kihonda pamoja na majengo mawili ya karakana za umeme wa magari na ufundı seremala umefikia hatua za kuanza kupauliwa.
- (iii) Ujenzi wa Karakana ya kisasa ya Useremala katika Chuo cha Ufundı Stadi cha Mkoa wa Dodoma kwa ajili ya ufundishaji na utengenezaji wa samani za kisasa uko katika hatua za mwisho. Karakana hii itatumika pia katika kutengeneza samani kwa ajili ya biashara na hivyo kukiongezea chuo mapato na kupunguza utegemezi kwa Serikali;

- (iv) Ukarabati wa awamu ya kwanza wa Chuo cha Ufundı Stadi cha Busokelo uliohusisha Karakana 3, Jengo la Utawala na Madarasa 2. Kwa sasa wanafunzi 60 wamedahiliwa katika Chuo hicho na kuanza mafunzo mwezi Machi, 2017 katika fani tatu (3) za Ubunifu, Ushonaji na Teknolojia ya Nguo; Useremala na Ufungaji Umeme;
- (v) Ukarabati wa Chuo cha Ufundı Stadi cha Nkowe kilichopo wilayani Ruangwa umefanyika na tayari Chuo kimepokea wanafunzi wa Mwaka wa Kwanza wapatao 28 katika Fani za Ufundı wa Umeme, Ujenzi, na Ushonaji. Tunatarajia baada ya ukarabati wa bweni la Wasichana kukamilika, idadi ya wanafunzi wa kike hasa katika fani ya Ushonaji itaongezeka; na
- (vi) imepata mkadarasi kwa ajili ya kukarabati Chuo cha Ufundı Stadi cha Wilaya ya Karagwe ambapo kazi itaanza rasmi mwezi Juni, 2017 baada ya kukamilika kwa taratibu za mkataba.
- (vii) kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu VETA ilifanya makubaliano ya kurasimisha ujuzi wa

- mafundi stadi 3,900 waliopata ujuzi nje ya mfumo rasmi wa mafunzo;
- (viii) imetoa mafunzo mbalimbali kwa Wakufunzi/Walimu, Watumishi wa VETA na Wajasiriamali wapatao 1,437 kuhusu kuandaa, kufundisha na kupima mitaala inayozingatia umahiri na masuala ya upatikanaji wa taarifa za kazi.

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu – (HESLB)

65. **Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ina jukumu la kutoa Mikopo kwa Wanafunzi wahitaji waliodahiliwa katika Taasisi za Elimu ya Juu kwa ajili ya masomo ya Shahada. Bodi pia ina jukumu la kukusanya marejesho ya mikopo iliyotolewa kwa Wanafunzi wa Taasisi za Elimu ya Juu. Katika mwaka 2016/17, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilifanya yafuatayo:

- (i) ilitoa mikopo kwa jumla ya wanafunzi **122,374** ambapo wanafunzi **28,785** ni wapya ambao mkopo wao unagharimu **Shs 104,613,516,187** na wanafunzi **93,559** ni wanaoendelea na masomo ambao unagharimu **Shs 379,180,441,499.**
- (ii) ilitoa ruzuku ya **Shs.**

4,627,160,700.00 kwa wanafunzi **1,584** wanaoendelea na masomo ndani ya nchi na **Shs. 811,091,544.00** kwa wanataaluma **44** wanaoendelea na mafunzo ya uzamivu nchini Ujerumani.

- (iii) ilitoa mikopo wanafunzi **448** wanaoendelea na masomo katika Vyuo Vikuu mbalimbali nje ya nchi ambapo jumla ya **Shs 5,362,054,708.00** zilitumika hadi kufikia **Aprili, 2017**.
- (iv) inaendelea kutekeleza mikakati ya kukusanya madeni ikiwa ni pamoja na utoaji elimu kwa wanufaika na waajiri kuhusu umuhimu na faida kurejesha mikopo kwa wakati.
- (v) imeendelea kuimarisha ushirikiano na Mamlaka nyingine hususan Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Wizara ya Fedha na Mipango, Mifuko ya Hifadhi za Jamii, Taasisi za Kifedha, Idara ya Uhamiaji na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) kwa lengo la kuwatambua Waajiri na Wanufaika Waajiriwa. Ushirikiano utawezesha kutumia Kanzi –Data za Taasisi nyingine ili kubaini wanufaika wengi zaidi.

66. **Mheshimiwa Spika**, Napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru waajiri kwa ushirikiano mkubwa wanaoutoa katika kuhakikisha wanufaika wa mikopo wanafanya marajesho kwa wakati. Aidha, nitumie fursa hii kuwataka wanufaika wote ambao hawajaanza kufanya marejesho kutekeleza wajibu huo mara moja ili kuepuka usumbufu wa kuchukuliwa hatua za kisheria.

Kituo cha Maendeleo Dakawa

67. **Mheshimiwa Spika**, Kituo cha Maendeleo Dakawa kina jukumu la kutunza na kuhifadhi majengo, vifaa, na miundombinu yote iliyokabidhiwa na chama cha ANC kwa ajili ya kulinda historia ya Ukombozi wa Afrika Kusini. Wizara yangu inao mpango wa kukiendeleza kituo hiki na kukitumia katika kutoa Elimu ya Sayansi, TEHAMA na Ufundi ili kukifanya kuwa Kitovu cha utoaji wa Elimu ya Sayansi na Teknolojia (Centre of Excellence for Science and Technology). Ili kutimiza azma hiyo katika Mwaka 2016/2017, Kituo cha Maendeleo Dakawa kimetekeleza yafuatayo;

- i. Kimeanza taratibu za kupata Hati Miliki ya Kituo kilichokabidhiwa kwa Serikali na chama cha ANC cha Afrika Kusini;
- ii. Kimefanya ukarabati na matengenezo ya mitambo ya kusukuma maji safi;

- na
- iii. Kimeanza maandalizi ya kuandaa Muundo wa Kisheria wa Uendeshaji wa Kituo.

Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs)

68. **Mheshimiwa Spika**, Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs) vina jukumu la kusimamia Mafunzo ya Ufundu Stadi na Elimu ya Wananchi kulingana na mahitaji ya jamii husika na kutengeneza Programu za Mafunzo hayo. Katika mwaka 2016/17 Wizara ilifanya yafuatayo:
- (i) ukarabati wa miundombinu ya Madarasa, Mabweni, Karakana pamoja na kutoa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDCs) vya Kasulu, Rubondo, Gera, Kisarawe, Karumo, Sengerema na Bariadi ili viweze kuendelea kutoa mafunzo ya ufundu stadi.
 - (ii) imesambaza vifaa vya ufundu katika fani za magari, umeme wa magari, umeme, uashi, useremala, uchomeleaji, ushonaji, fotokopia, na kompyuta ili kuimarisha ufundishaji.
 - (iii) Imefanya kikao na Wakuu wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi hapa Dodoma tarehe 3 Machi, 2017

ambapo changamoto za Vyuo hivi zilijadiliwa zikiwemo uchakavu wa miundombinu, uboreshaji wa mitaala, migogoro ya ardhi, madeni ya wazabuni na madai ya Watumishi. Maazimio 17 yalitolewa na yanafanyiwa kazi ili kutatua changamoto zilizopo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi.

Chuo Kikuu Cha Ushirika Moshi

69. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/17 Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi kimefanya ukarabati wa ofisi 11 za Mikoa ili kuboresha usimamizi wa ofisi za Mikoa kwa kupitia mradi wa *Market Infrastructure, Value Addition and Rural Finance Support (MIVARF)*. Ukarabati uliofanyika na uwekaji wa samani umegharimu Jumla ya **shilingi 230,780,457.00**. Aidha, Chuo kimefanya ukarabati wa vyumba vya mihadhara, mabweni, nyumba za makazi ya wahadhiri na ofisi. Kazi hii imeboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia katika Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi.

Chuo Kikuu Cha Mzumbe

70. **Mheshimiwa Spika**, katika Chuo Kikuu cha Mzumbe Wizara imefanya ukarabati na ujenzi wa miundombinu kwenye Kampasi ya Mbeya wenye thamani ya

Shilingi bilioni 1.5. Aidha, uimarishaji wa miundombinu umeendelea kwa kujenga Jengo la Taaluma na Utawala ambalo litagharimu **shilingi bilioni 2.7.** Hadi sasa Serikali imeshatoa **shilingi milioni 800** kwa ajili ya ujenzi huo. Aidha, Chuo kimepokea mkopo wa **shilingi Milioni 500** kutoka TEA kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo. Kazi zilizokwishafanyika ni pamoja na ujenzi wa msingi, nguzo na jamvi ghorofa ya kwanza. Kukamilika kwa kazi hizi kutaongeza fursa za masomo kwa wanafunzi wa fani za uongozi na kuboresha mazingira ya kufundishia na ujifunzaji katika Kampasi ya Mbeya.

Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa

71. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/2017 Wizara yangu kupitia Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa kimetekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kimeongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 3,682 mwaka 2015/2016 hadi kufikia wanafunzi 4,135 mwaka 2016/2017, wakiwemo wanawake 886 ambao ni sawa na asilimia 24;
- (ii) Kimefanya ukarabati wa maeneo ya kujifunzia kwa kujenga madawati ya kujisomea (*reading platforms*);
- (iii) Kimeazisha shahada ya uzamili katika

Sayansi na Elimu kwa masomo ya Biolojia na Kemia; na

- (iv) Kimefanya ukarabati wa mabweni ya wanafunzi na kuendelea na ujenzi wa ukumbi wa miadhara;

Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania (OUT)

72. **Mheshimiwa Spika**, Kimekamilisha ukarabati wa Kituo cha Chuo Kikuu Huria cha Tanzania cha Geita kwa kuboresha kumbi za Miadhara na Ofisi za Wahadiri, kazi iliyogharimu **Shilingi milioni 31.2**. Aidha, ukarabati wa miundombinu unaendelea katika Kituo cha Mwanza kwa kuongeza kumbi za Miadhara na Vyumba vya mitihani, ambapo **Shilingi milioni 100** zimetumika. Ukarabati wa Vituo hivi utaboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia na hivyo kutoa Elimu yenye ubora zaidi.

Baraza la Mitihani la Tanzania – NECTA

73. **Mheshimiwa Spika**, Baraza la Mitihani la Tanzania lina jukumu la kuendesha Mitihani ya Taifa na kutunuku vyeti kwa wahitimu. Katika mwaka 2016/17, limefanya kazi zifuatazo:

- (i) limeendesha upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne uliofanyika mwezi Novemba, 2016 ambapo jumla ya watahiniwa 1,017,776 walifanya mtihani kati ya 1,054,191 waliokuwa

- wamesajiliwa. Upimaji wa Kitaifa wa Kidato cha Pili ambapo, jumla ya watahiniwa 410,519 walifanya upimaji huo kati ya 435,075 waliokuwa wamesajiliwa;
- (ii) limeendesha Mtihani wa Taifa wa Kumaliza Elimu ya Msingi Mwaka 2016 ambapo jumla ya watahiniwa 789,479 walifanya mtihani huo kati ya 795,739 waliokuwa wamesajiliwa; pamoja na Mitihani ya Kidato cha Nne na Maarifa ambapo jumla ya watahiniwa 414,608 walifanya mitihani hiyo kati ya 429,033 waliokuwa wamesajiliwa.
- (iii) limekamilisha usajili wa watahiniwa wa Kidato cha Sita (ACSEE) 2017 ambapo jumla ya watahiniwa 74,801 wanaendelea kufanya Mtihani huo ulioanza tarehe 2 Mei, 2017.
- (iv) limeimarisha usalama wa mitihani na kurahisisha kazi ya ufungaji wa mitihani ya Taifa kwa kununua mashine ya Kielektroniki ya kuhesabu na kufunga karatasi za mitihani (*poly wrapping and Packing machine*).
- (v) Imekamilisha kazi ya kuunda mfumo wa Kompyuta utakaotumika

kuwasajili wanafunzi wote wa shule za msingi nchini. Katika mfumo huu, kila mwanafunzi atasajiliwa na kupatiwa namba ya pekee ya utambulisho ambayo itamtambulisha katika hatua zote za mafunzo atakazoendelea nazo.

- (vi) Lilifanya uhakiki wa vyeti vyatatu wa umma wa Serikali za Mitaa, Taasisi/Mashirika ya Umma, Wakala wa Serikali na taarifa yake kukabidhiwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (TEWW)

74. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kupitia Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ina jukumu la kutekeleza Sera ya Elimu ya watu Wazima na Elimu Nje ya Mfumo Rasmi. Katika mwaka 2016/2017 Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima imeteketeza kazi zifuatazo;

- (i) Imejenga kumbi mbili za miadhara na ofisi mbili za wafanyakazi katika Kampasi ya Morogoro (WAMO). Ujenzi upo katika hatua ya kupaua;
- (ii) Imefanya ukarabati wa Madarasa mawili yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 50 kila moja, Jengo la utawala, Jengo la Maktaba, Chumba

- kimoja cha Mgahawa, chumba cha Kompyuta, bweni moja na vyoo vya wanafunzi katika Kampasi ya Luchelele Mwanza;
- (iii) Imedahili wanafunzi 855 katika program za muda mrefu za Shahada, Stashahada na Astashahada;
 - (iv) Imenunua Vitabu 346 kwa ajili ya mafunzo ya Shahada na Stashahada na kuwekwa katika maktaba za TEWW Dar es salaam (120) na Mwanza (226); na
 - (v) Imesajili vituo vipyta 72 vinavyotoa Elimu ya Sekondari nje ya mfumo rasmi na kufanya jumla ya vituo kuwa 420.

Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)

75. **Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu una majukumu ya kuandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika uongozi na uendeshaji wa elimu; kufanya utafiti, kuandaa na kusambaza makala na vitabu pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu katika mambo yanayohusu uongozi na uendeshaji wa elimu. Katika mwaka 2016/17, ADEM ilifanya shughuli zifuatazo:

- (i) imekarabati majengo 2 ya mihadhara na mfumo wa umeme, kufunga viti na meza 831 na kununua seti ya Komputa 117 kwa ajili ya uendeshaji wa mafunzo katika Kampasi ya Bagamoyo.
- (ii) iliandaa na kuendesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu katika uongozi na uendeshaji wa elimu ambapo imetoa mafunzo ya Cheti cha Uongozi na Usimamizi wa Elimu (CELMA) kwa Walimu Wakuu 706 kutoka Mikoa ya Iringa, Mbeya, Njombe na Songwe.
- (iii) imetoa mafunzo ya Usimamizi wa Shule na ujenzi wa miundombinu na majengo kwa Wakuu wa Shule 1,200.
- (iv) imetoa mafunzo kuhusu usimamizi wa elimu katika ngazi ya shule kwa wajumbe 129,609 wa Kamati za Shule za Msingi zipatazo 11,647 kwenye Mikoa 19.
- (v) imenunua magari 3 kwa ajili ya matumizi ya Wakala na imefadhili watumishi 3 masomo ya Shahada ya Uzamivu ambao wanaendelea na masomo kwenye Vyuo vya hapa nchini.

Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania

76. **Mheshimiwa Spika**, Huduma bora za Maktaba zinachangia katika utoaji wa Elimu bora katika nchi yoyote ile. Wizara yangu katika mwaka 2016/17 kupitia Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania imefanya kazi zifuatazo:

- (i) imewezesha upatikanaji wa vitabu 68,801, magazeti 10,698 na majarida 461.
- (ii) imeendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uanzishaji, upangaji na uendeshaji wa Maktaba za shule na vyuo katika shule 88, (msingi 46 na sekondari 42), katika Jiji la Dar es Salaam na katika Taasisi za *All Together in Dignity to Overcome Poverty* Awali na Msingi (ATD), Mahabusu ya Watoto ya Jiji la Dar es Salaam, Ubalozi wa Marekani, *Tanzania House of Talent* (THT), *Fore Plan Clinic* na *Alliance Francee Library*.
- (iii) imeimarisha maktaba 43 kwenye Mikoa na Halmashauri kwa kuanzisha *reading corners* za kujifunzia stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

77. **Mheshimiwa Spika**, Naomba nitumie fursa hii kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge

tushirikiane kuhimiza Halmashauri zote nchini pamoja na Wadau kuona umuhimu wa kuanzisha Maktaba na kuhamasisha wananchi kujenga utamaduni wa kusoma Vitabu, Vitarida na Machapisho mbalimbali. Wizara yangu iko tayari kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu uanzishwaji na uendeshaji wa Maktaba.

Mamlaka ya Elimu Tanzania – TEA

78. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA) ina jukumu la kusimamia Mfuko wa Elimu na kuhamasisha uchangiaji ili kuongeza nguvu za Serikali katika kugharamia miradi ya elimu. Katika mwaka 2016/17 Mamlaka ya Elimu Tanzania ilifanya kazi zifuatazo:

- (i) ilifuatilia katika shule 40 za Msingi na Sekondari katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro na Iringa zilizopatiwa vifaa vya kuboresha mazingira ya elimu vikiwemo madawati, vifaa vya TEHAMA na mabati ili kuhakiki ubora wa vifaa, matumizi na hatua za utekelezaji wa miradi kulingana na kiasi cha fedha kilichotolewa.
- (ii) ilifuatilia miradi 15 inayoendelea ya ujenzi wa nyumba za walimu katika shule za sekondari za Uleling'ombe - Kilosa, Luegu - Namtumbo, Isanzu

- Mkalama, Kinamapula - Ushetu, Ndoloeleji - Itilima, Kandawale - Kilwa zilizopo katika maeneo magumu kufikika ili kuhakiki maendeleo ya kazi za ujenzi.

Tume ya Taifa ya UNESCO

79. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Taifa ya UNESCO ina majukumu ya kuratibu na kutekeleza Programu za UNESCO nchini katika nyanja za Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi Jamii, Utamaduni, Mawasiliano na Habari. Katika mwaka 2016/17, Tume ya Taifa ya UNESCO imeandaa, imechapisha na kusambaza nakala 700 za Jarida la Tanzania na UNESCO Toleo namba 13, imefadhili Walimu 35 wa shule za sekondari waliopata Mafunzo ya juu ya *Competence Based Assessment*, imefanya mikutano kupitia Kamati za kitaifa ili kuboresha mahusiano na utekelezaji wa programu za UNESCO na kuratibu mkutano wa vijana wa kikanda pamoja na mikutano mingine ili kuwajengea uwezo katika masuala ya amani, uongozi na stadi za kimaisha.

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)

80. **Mheshimiwa Spika**, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) lina jukumu la kusimamia Ithibati na Uthibiti Ubora wa Elimu ya Ufundi nchini. Katika mwaka

2016/17, NACTE ilifanya kazi zifuatazo:

- (i) Ilidahili wanafunzi 96,694 wa elimu ya ufundi katika Vyuo 551 vilivyosajiliwa na NACTE.
- (ii) Ilihakiki Mitaala 15 ya Programu za Mafunzo kutoka Vyuo 4 vya Elimu ya Ufundii;
- (iii) iliidhinisha mitaala 9 inayozingatia mahitaji ya soko la ajira na viwango vya Kitaifa na Kimataifa iliyoandalialiwa na Taasisi ya Ustawi wa Jamii, Chuo cha Bahari Dar es Salaam, na Chuo cha Taifa cha Usafirishaji.
- (iv) ilifanya *post validation* kwa Mitaala 16 kutoka Vyuo 5 vya Elimu ya Ufundii na ilifanya uhakiki wa awali (prevalidation) kwa Mitaala 45 ya Programu mbalimbali za mafunzo.
- (v) iliandaa mfumo wa udahili na kuchakata matokeo ya Watahiniwa Kanuni na Miungozo ya Uthibiti wa Ubora wa Rasilimali Watu katika Vyuo vya Elimu ya Ufundii nazo ziliandaliwa.
- (vi) itaendelea kutengeneza na kuboresha mifumo ya kieletroniki itakayosaidia kuhakikisha ubora wa Elimu ya Ufundii ikiwemo Mifumo ya ukusanyaji wa takwimu za

wanafunzi; usimamizi wa rasilimali watu Vyoni na mfumo wa kutoa vyeti na *transcript* kwa Wanafunzi wa Vyuo vya Elimu ya Ufundu.

- (vii) ilikagua Vyuo 88 vya Elimu ya Ufundu na kufanya tathmini juu ya ubora wa utoaji wa mafunzo ambapo baadhi ya vyuo vilifungiwa kwa sababu mbalimbali
- (viii) itaendelea kuimarisha Ofisi za Kanda ikiwemo kuwaongezea Nguvukazi na vitendea kazi ili kuwafikishia walengwa wote huduma bora. Wizara inategemea kufanya utafiti katika maeneo yanayohusu utoaji wa Elimu ya Ufundu na kutoa ushauri stahiki ili kuhakikisha elimu ya ufundi inakidhi haja ya soko la ajira.

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania

81. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania ina jukumu la kuhakiki ubora wa Elimu ya Juu kwa kutoa Ithibati. Katika mwaka 2016/17 Tume ya Vyuo Vikuu ilifanya yafuatayo:

- (i) iliratibu mfumo wa udahili wa pamoja ambapo jumla ya wanafunzi 69,539 walidahiliwa. Idadi hii iliongezeka ikilinganishwa na mwaka 2015/16 ambapo walidahiliwa wanafunzi

64,919. Aidha, kati ya wanafunzi hao waliodahiliwa mwaka 2016/17 wanafunzi 44,765 wako katika Vyuo vyaa Serikali na 24,774 katika vyuo binafsi (*Kielelezo 11a na 11b*).

- (ii) imeendelea kusimamia ubora wa Elimu ya Juu kwa kukagua Vyuo Vikuu 98 ili kuhakiki Ubora wa Mitaala, ufundishaji vyuoni na uwezo wa vyuo katika utoaji wa Elimu ya Juu nchini. Maeneo yaliyozingatiwa katika ukaguzi huo ni pamoja na uwepo wa Wahadhiri wa kutosha na wenyе sifa, uwepo wa miundombinu stahiki, uwepo wa vifaa vyaa kufundishia na kujifunzia, uwezo wa maabara na karakana kulingana na mahitaji ya mafunzo husika pamoja na uongozi wa Vyuo. Aidha, Vyuo vilivyobainika kuwa na kasoro vitaendelea kuchukuliwa hatua kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu;
- (iii) ilishiriki kwenye vikao vyaa kikanda vinavyohusiana na Elimu ya Juu ikiwa ni pamoja na vikao vyaa *Inter – University Council for East Africa, Southern Africa Development Community* na Kamati ya Ufundi ya Elimu ya Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa lengo la kupata uzoefu na kuongeza weledi katika kusimamia

- ubora wa Elimu ya Juu;
- (iv) imeendelea kuratibu utoaji wa ufadhili kwa wahadhiri 44 wanaoendelea na masomo ya ngazi ya uzamivu nchini Ujerumani;
- (v) ilifanya ukaguzi wa Chuo Kikuu kinachopendekewa kuanzishwa cha Greenbird kilichopo Mwanga, Mkoani Kilimanjaro na kubaini kuwa hakijakidhi vigezo vyta kuwa Chuo Kikuu.
- (vi) ilitambua Tuzo 547 za ngazi mbali mbali zilizotolewa katika Vyuo vyta Elimu ya Juu nchi za nje;
- (vii) iliandaa Maonesho ya 11 ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia ambapo Vyuo vyta Elimu ya Juu sitini (60) vyta ndani na nje ya nchi vilishiriki.

Chuo Cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA)

82. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA) kina jukumu la kutoa mafunzo katika Fani za Sayansi Jamii, kufanya utafiti; na kutoa ushauri. Katika mwaka 2016/2017 kilitekeleza majukumu yafuatayo:

- (i) Kimeandaa mitaala minne ya Ngazi ya Shahada katika fani za Elimu.

- (ii) kimeandaa Mitaala na Vifaa vya ufundishaji wa Stashahada ya Elimu ya Msingi; Stashahada ya Maktaba na Habari na kiliwezesha Wahadhiri 44 kupata mafunzo kwa lengo la kufundisha kwa ufanisi Stashahada ya Elimu ya Msingi na Stashahada ya Maktaba na Habari.
- (iii) kimeandaa Mitaala ya Shahada za Uzamili za Miradi na Usimamizi *Master in Project Planning and Management, Human Resources Management, Educational Planning and Administration na Gender and Development* pamoja na mafunzo kwa Kozi fupi 6 juu ya maadili na uongozi na
- (iv) kimechapisha Tafiti 37 katika Majorida ya Kimataifa ya Tafiti za Kisayansi.

Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH)

83. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) ina jukumu la kuratibu na kuendeleza utafiti na ubunifu nchini. Aidha, Tume hiyo imepewa jukumu la kisheria la kusimamia Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji Sayansi na Teknolojia (MTUSATE). Katika kukuza na kuendeleza teknolojia nchini COSTECH imefanya yafuatayo:

- (i) Imekamilisha maandalizi ya kufungua kumbi za ubunifu (innovation spaces) na Atamizi/*Virtual Incubator* katika Mikoa ya Mwanza na Iringa. Vyuo Vikuu vya Dodoma, Dar es Salaam, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela na Zanzibar State University (SUZA) vimeelekezwa kuanzisha atamizi ili kukuza ubunifu miongoni mwa vijana. Atamizi hizi zinachochea uendelezaji wa ubunifu katika sekta mbalimbali na kuongeza ajira kwa vijana;
- (ii) imeendelea kufadhili Watafiti 27 wanaoendelea na mafunzo ya Shahada ya Uzamili (4) na Uzamivu (23);
- (iii) kwa kushirikiana na Taasisi ya Teknolojia ya Denmark, imetoa elimu juu ya miliki ubunifu na uhawilishaji wa teknolojia (intellectual property right) kwa watafiti na wanasayansi (30) toka taasisi za utafiti na elimu ya juu. Mafunzo hayo yanalenga kuwawezesha watafiti kulinda ubunifu wao;
- (iv) Imefadhili miradi ya tafiti 18 katika maeneo ya Viwanda, Afya, Kilimo, Mifugo na Maliasili ili matokeo ya utafiti yaweze kuleta majawabu ya changamoto katika jamii;

- (v) Kupitia mfuko wa MTUSATE imefadhili wanafunzi (2) wanaoendelea na mafunzo ya uzamili (4) na uzamivu (23). Aidha COSTECH imeanza utaratibu wa kudahili wanafunzi wapya (50) kujiunga na shahada ya uzamili (35) na uzamivu (15);
- (vi) Ili kufanikisha usambazaji wa matokeo ya utafiti yaweze kuwafikia wadau wengi, COSTECH imeanza ukarabati wa chumba cha studio maalum kwa ajili ya kuandaa vipindi vya redio, televisheni na machapisho ya kisayansi katika ili viweze kurushwa katika vyombo mbalimbali vya habari. Kwa lengo la kuhimiza utamaduni wa kutumia sayansi, teknolojia na ubunifufuu katika kutatua matatizo yanayoikabili jamii; na
- (vii) imefanyika ukarabati na kununua vifaa vya maabara katika Kituo cha Utafiti wa Uvuvi (TAFIRI – Sota) kilichopo mkoa wa Mara. Aidha, ukarabati wa Taasisi ya utafiti wa mifugo Tanga (TALIRI) unaendelea. Ukarabati huu utaboresha miundo mbinu ya utafiti na kufanya matokeo ya utafiti yawe na ubora zaidi.

Chuo cha Ufundi Arusha

84. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/17, Chuo cha Ufundi Arusha kilitekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Kimeandaa mtaala utakaotumika katika Kituo cha Kikuletwa kutoa Mafunzo ya Ufundi Stadi Ngazi ya Cheti katika fani za *Hydropower Maintenance; Domestic Electrical Installation; Plumbing and Pipe fitting; na Blockwork and Masonry;*
- (ii) Kimetoa mafunzo ya ukarabati wa Miundombinu pamoja na Mitambo ya kuzalisha umeme utokanao na nguvu za maji *Hyropower* kwa Wanataluma 19 wa Chuo ili kuwajengea uwezo, zaidi katika fani zao;
- (iii) Kimekamilisha mchakato wa kuanzisha mafunzo Ufundi Sanifu Ngazi ya Stashahada ambayo yanatarajiwa kuanza Mwezi Oktoba, 2017 katika fani ya *Electrical and Hydropower Maintenance;*
- (iv) Kimeanza kufanya Usanifu wa jengo lenye Madarasa na Maabara za Programu za Madini na Vito, Uhandisi wa Vifaa Tiba, Uhandisi wa Mawasiliano ya Anga na Teknolojia ya Mawasiliano ya Habari katika Chuo

cha Ufundu Arusha ili kuongeza udahili katika fani hizo;

- (v) Kimefanya tafiti zinazolenga kuendeleza matumizi ya teknolojia ya umwagiliaji wa matone kwa kutengeneza vifaa ambavyo matundu yake hayazibi kirahisi ili kuimarisha maendeleo ya kilimo cha umwagiliaji katika maeneo yenye ukame;
- (vi) kimeendelea kupima uimara wa udongo, kokoto na lami zinazotumika katika ujenzi wa barabara ili kuanisha ubora wake na kutoa ushauri wa matumizi sahihi wakati wa ujenzi wa barabara;
- (vii) Kimeendelea kuboresha fimbo inayowasidia walemavu wa macho (electronic blind stick) katika kutambua sehemu za mapitio yao ili kuwaongoza kwa urahisi na kwa gharama nafuu;
- (viii) Kimefanya ukarabati wa Jengo la zamani katika Chuo cha Ufundu Arusha kwa kulibadili matumizi yake ili kiwe kituo cha kufundishia stadi za kazi katika ufundu bomba, ufundu rangi na ufundu uashi. Jengo hilo lina uwezo wa kuchukua wanafunzi 94 kwa wakati mmoja na litaongeza idadi ya mafundi mahiri;

- (ix) Kimeendelea na utekelezaji wa Mradi wa ukarabati wa miundombimu kwa ajili ya kuendeleza Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Nishati Jadidu pamoja na uzalishaji Umeme utokanaao na Maji katika kituo cha kikuletwa kilichopo Wilayani Hai;
- (x) Kimekamilisha ujenzi wa Majengo mapya 4 na ukarabati wa majengo saba (7) ya zamani;
- (xi) Kimekamisha Mpango Kazi wa Biashara (*Business Plan*) wa kuanzisha Kampuni ya Kikuletwa *Power Public Company Limited* (KPPCL) inayomilikiwa na Chuo cha Ufundis Arusha kwa ajili ya kushughulikia uzalishaji umeme katika Kituo cha Kikuletwa umekamilika; na
- (xii) Kinaendela kuunda Helikopta ya gharama nafuu na salama kwa safari fupi nchini ili kurahisisha usafiri katika maeneo yasiyofikika kwa magari.

Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam - (DIT)

85. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/2017 Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam imefanya shughuli zifuatazo:

- (i) imeendelea kutoa mafunzo ya teknolojia kwa wanafunzi na wafanyakazi wa viwandani ili waweze

- kuongeza ujuzi mpya katika taaluma mbalimbali;
- (ii) imeanzisha kozi ya Stashahada ya Ufundı Sanifu Maabara kwenye Kampasi ya Mwanza; Kozi hii itazalisha wataalam ambao watasaidia kukabiliana na uhaba wa mafundi sanifu wa maabara katika shule za sekondari, hospitali, vituo vya afya na zahanati; pamoja na kuongeza Mafundi Sanifu wanaohitajika katika viwanda vilivyopo na vitakavyoanzishwa hapa nchini;
- (iii) imefanya ukarabati wa miundombinu ya karakana ya magari katika Taasisi ya Teknolojia ya Dar es Salaam kwa kununua na kusimika mashine ya kisasa ya utambuzi wa matatizo ya magari; na
- (iv) imekamilisha ujenzi wa *Teaching Tower Complex*. Jengo hili litakuwa na uwezo wa kuhudumia wanafunzi 984 kwa wakati mmoja hivyo litasaidia kuongeza udahili wa wanafunzi wa kozi mbalimbali za sayansi na teknolojia ambao unahitajika sana kuiwezesha Serikali kufikia azma yake ya kujenga uchumi wa viwanda.

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya

86. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2016/17, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya kilitekeleza majukumu yafuatayo:
- (i) Kilikamilisha Mtaala wa kufundishia fani mpya ya stashahada ya *Highway Engineering* katika Chuo cha Sayansi Teknolojia Mbeya na mafunzo yameanza kutolewa kwa wanafunzi 14 waliodahiliwa; Utoaji wa mafunzo katika fani hiyo utasaidia kuongezeka upatikanaji wa wataalamu na wahandisi wa miundombinu ya barabara ambapo kwa sasa kuna uhaba mkubwa;
 - (ii) Kimekamilisha mitaala ya Stashahada, Shahada ya Uzamili na Uzamivu katika maeneo ya *Automotive Engineering, Oil and gas safety and reliability Engineering, Renewable Energy Engineering, Structural Engineering, Civil engineering* na *Water Resources Engineering*. Uanzishwaji wa mafunzo haya utasaidia kuongeza idadi ya wanafunzi wapatao 240 kwa mwaka na hivyo kuongeza wataalamu mbalimbali hususani katika fani ya

- Mafuta na Gesi ambayo ina uhaba wa wataalamu na hivyo inategemea zaidi wataalamu kutoka nje ya nchi;
- (iii) Kimeandaa Mitaala ya mafunzo ya Shahada za *Laboratory Science and Technology na Biomedical Equipment Engineering*;
 - (iv) Kiliimarisha ufundishaji na ujifunzaji kwa kufadhili Watumishi 94 katika mafunzo ya muda mrefu ngazi ya Shahada ya Kwanza, Uzamili na Uzamivu ili kuwawezesha watumishi kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi;
 - (v) Kimeanzisha atamizi ya teknolojia kwa ajili ya kuchochea ubunifu na maendeleo ya teknolojia. Atamizi hii inajikita katika maeneo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Uundaji wa mitambo na vifaa mbalimbali, Sayansi na Biashara. Atamizi hii ni chachu ya kuleta maendeleo ya viwanda katika sekta ya uchumi na Biashara pamoja na kuongeza ubunifu na ajira kwa vijana.

Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania

87. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Nguvu za Atomiki ina jukumu la kusimamia na kudhibiti matumizi salama ya mionzi. Katika mwaka 2016/17 imetekeleza

majukumu yafuatayo:

- (i) imechambua maombi 244 ya uingizaji nchini, usafirishaji na utumiaji wa vyanzo vya mionzi ili kubaini kama maombi hayo yanakidhi matakwa ya Sheria Na. 7 ya Nguvu za Atomiki ya Mwaka 2003. Uchambuzi huo unahusisha chanzo cha mionzi, sifa za kitaaluma za msafirishaji na mtumiaji wa chanzo cha mionzi *operator*, mpango wa uhifadhi wa kudumu wa mabaki ya chanzo husika na mpango wa kudhibiti endapo janga linalohusisha chanzo cha mionzi litatokea;
- (ii) imekagua vituo 131 vinavyotumia vyanzo vya mionzi kwa kuangalia ubora wa jengo la kuhifadhi au kutumia chanzo cha mionzi, ubora wa chanzo chenyewe cha mionzi, sifa za kitaaluma za mtumiaji wa chanzo cha mionzi (*Operator*) na usahihi wa taarifa za nyaraka za chanzo cha mionzi na kutoa ushauri kwa lengo la kuhakikisha usalama kwa watumiaji, raia na mazingira. Kati ya vituo 131, vituo 102 vilikidhi matakwa ya sheria, vituo 26 vilikutwa na dosari kadhaa na zikapewa muda kurekebisha kasoro hizo na vituo 2 vilifungiwa baada ya kuona

- vimekiuka matakwa ya sheria kwa kiasi kikubwa na kituo kimoja (1) kimesitisha chenyewe utoaji huduma ya uchunguzi wa magonjwa.
- (iii) imekamilisha Taarifa sita (6) za kituo cha kupima viasili vya mionzi kwenye hewa ya anga kijulikanacho kama “*Radionuclide Monitoring Station-RN64*” kilichopo katika jengo la Idara ya Fizikia katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuzituma kwenye Shirika la Kimataifa la Kuzuia Majaribio ya Silaha za Kinyuklia lenye Makao Makuu Vienna Austria. Taarifa hizo zilionyesha kuwa katika kipindi hicho kulikuwa hakuna uchafuzi wa mazingira unaotokana na majaribio ya kinyuklia. Vilevile, taarifa hizo zilionyesha viwango vya kawaida vya chembechembe za vyanzo asili vya mionzi ambavyo havina athari yoyote kwa binadamu na mazingira;
- (iv) ilifungua ofisi zake katika miji ya Songea, Sirari na Mtwara kwa lengo la kuimarisha usimamizi na udhibiti wa mionzi katika mipaka ya nchi;
- (v) imefanya upembuzi wa awali (*Geophysical survey*) na michoro sanifu ya kiuhandisi ya ujenzi wa

Maabara ya Kisasa ya upimaji wa viwango vya mionzi kwa binadamu na mazingira katika eneo la Tume ya Nguvu za Atomiki huko Arusha. Ujenzi wa maabara hii ya Tume utaboresha utoaji wa huduma, utafiti, kuongeza mapato na ufanisi katika utekelezaji wa majukumu ya TAEC.

Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha – NM-AIST

88. **Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojiaya Nelson Mandela ina jukumu la kutoa Elimu na Mafunzo katika ngazi ya Uzamili na Uzamivu pamoja na kufanya utafiti katika ngazi ya Ubobezi. Katika mwaka 2016/17, NM-AIST ilitekeleza kazi zifuatazo:

- (i) Imekamilisha ujenzi wa kituo cha kuendeleza Ubunifu na Ujasiriamali katika fani ya TEHAMA *ICT Resource Centre* na kuweka mifumo ya TEHAMA kwenye Kituo hiki imemalizika na kitahudumia wanafunzi wasiopungua 30 kila mwaka;
- (ii) Imekamilisha michoro na makisio ya gharama ya ujenzi wa jengo la Idara ya Miliki na uwanja wa mahafali; na imekamilisha kazi ya kuweka mipaka ya ardhi eneo la Karangai kwa asilimia 80; na

- (iii) Imeanza utekelezaji wa Mradi wa Vituo viwili mahiri vya Taaluma na Utafiti *African Centres of Excellence* wenyewe thamani ya takriban **USD 12,000,000**; ambapo wanafunzi 29 wa Shahada za Uzamili na Uzamivu wamesajiliwa. Kati ya vituo hivyo, kimojawapo ni kwa ajili ya kuwa mahiri kwenye masuala ya maji, nishati na usafi wa mazingira wakati kituo cha pili kinajenga umahiri katika Kilimo lishe na usalama wa chakula. Vile vile, Vituo hivi vitaongeza fursa za kufanya utafiti, kuimarisha ufundishaji na kujenga uhusiano mzuri kati ya Taasisi na sekta binafsi.
- (iv) Imeanza utekelezaji wa mradi wa kuongeza uwezo wa tafiti za sayansi na teknolojia Afrika uliofadhiliwa na Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) wenyewe thamani ya Shilingi **bilioni 8.2**. Kupitia mradi huu wanafunzi 51 wa Uzamili na Uzamivu wamedahiliwa;
- (v) imekamilisha Mtaala wa Shahada ya Uzamili katika utafiti wa Afya ya Jamii (*Masters in Research of Public Health -MRPH*) na tayari umeshafanyiwa ithibati tayari kwa matumizi. Mtaala huu utaanza kutumika kwenye udahili mwaka 2017/18;

- (vi) Imefanya tafiti zilizolenga kutambua mambo yafuatayo:
- (a) magonjwa ya wanyama ambayo yana uwezekano wa kuambukiza wanadamu ili kudhibiti maambukizi ya maradhi ya wanyama kwenda kwa binadamu;
 - (b) magonjwa ya wanyama kupitia nyama yanayoweza kuambukiza binadamu ili kudhibiti maambukizi ya magonjwa ya wanyama kupitia nyama;
 - (c) mapungufu ya teknolojia ya kuchuja maji kwenye maeneo yenye upungufu wa miundombinu ya maji kwa wananchi Mkoani Arusha na kuiboresha ili kupata huduma ya maji safi na salama; na
 - (d) magonjwa ambayo yana uwezekano wa kuathiri afya za mifugo ili kuboresha afya za mifugo.

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

89. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kimefanya kazi zifuatazo:

- (i) Kimefanya tafiti zilizolenga

kutengeneza teknolojia rahisi ya kutenganisha madini ya shaba ili kuwawezesha Mafundi Mchundo na Wachimbaji wadogo wadogo kutenganisha shaba kwa ufanisi na tija; Kufuatilia mienendo ya Tembo kwa kutumia teknolojia ya *Global Position System* katika maeneo Hifadhi za Mayowosi, Igosi, Ugalla, Uyungu, Gisima, Luganzo na Gombe kwa lengo kudhibiti mauaji ya Tembo yanayotokana na ujangili; Kutengeneza mfumo wa ukusanyaji wa takwimu za afya vijiji na katika vituo vya afya nchini ili kuboresha ufuatiliaji na tathmini ya huduma za afya vijiji; na

- (ii) Kimefanya ukarabati wa bweni namba 1, 3, 4, 5, 6 na 7 ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa kurekebisha mifumo ya maji safi na maji taka. Aidha, uwekaji wa samani na ukarabati wa miundombinu ya kufundishia kama vile vyumba vya miadhara, vyumba vya semina na ofisi za walimu umefanyiwa kazi iliyogharimu jumla ya Shilingi **bilioni 1.2.**

Chuo Kikuu cha Dodoma

90. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Chuo Kikuu cha Dodoma kimefanya tafiti zifuatazo:

- (i) Kuainisha matumizi ya mtandao wa simu za mkononi katika ufuatiliaji wa ubora wa dawa katika mnyororo wa usambazaji (Pharmaceutical Supply Chain in Tanzania) ili kuboresha usambazaji wa dawa nchini;
- (ii) Kutambua malisho bora ya kuku wa kienyeji katika wilaya za Kongwa na Kiteto ili kuongeza uzalishaji wa kuku walioboreshw na hivyo kuimarisha hali ya kipato cha kaya kwa wananchi wanaoishi maeneo yenyе ukame;
- (iii) Kutambua usugu wa vimelea vya magonjwa katika maeneo yanayozunguka mbuga ya Serengeti ili kudhibiti magonjwa hayo na kuongeza uzalishaji wa wanyama wanaofugwa katika eneo hilo; na
- (iv) Kuanza utafiti wa Kuunda Mfumo wa Upimaji wa Stadi za Kuandika, Kusoma na Kuhesabu (KKK) na kuandaa maudhui ya Kielektroniki ili kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo

91. **Mheshimiwa Spika**, katika mwaka 2016/17 Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo cha kimefanya tafiti zifuatazo:
- (i) Kupunguza madhara yanayotokana na panya waharibifu wa mazao kwa kutumia harufu ya mkojo wa paka (*Felissilvestricatus urine*); kwa lengo la kuboresha uhifadhi wa mazao;
 - (ii) Kuongeza uzalishaji wa zao la maharage kwa kuongeza kinga na ustahimilivu wa maradhi ya virusi (Angular Leaf Spot na Bean Common Masaic Virus) na bakteria (Common Bacterial Blight) kwa lengo kuinua kipato cha kaya za vijijini hasa wanawake;
 - (iii) Kutambua vyakula vya samaki vinavyotokana na mimea ya asili ili kuongeza uzalishaji wa samaki kwa ajili maendeleo endelevu ya kilimo cha samaki nchini;
 - (iv) Kutambua vimelea kinga (vaccine) kwa ajili ya magonjwa ya nguruwe ili kuongeza uzalishaji, kuinua kipato na lishe bora katika kaya;
 - (v) Kuzuia madhara ya magonjwa ya brucellosis na Homa ya Bonde la Ufa (Rift Valley Fever) kwa Wanyama

wanaofugwa kwa kubuni madawa ya kinga ili kuimarisha afya za Wanyama hao; na

- (vi) Kuzuia magonjwa ya kupumua kwa kuku wa kienyeji (control of respiratory diseases) kwa kubuni chanjo ya magonjwa hayo ili kuongeza uzalishaji na kuinua kipato cha kaya za vijiji hasa wanawake.

Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi Shirikishi – Muhimbili

92. **Mheshimiwa Spika**, Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi Shirikishi –Muhimbili kimefanya tafiti zifuatazo:

- (i) Kuainisha matumizi sahihi ya dawa ya mseto katika kudhibiti na kutibu ugonjwa wa malaria na hivyo kuongeza usalama kwa watumiaji wa dawa hizo;
- (ii) Kutambua magonjwa ambayo yana uwezekano wa kuathiri afya ya Wanawake wajawazito na Watoto wachanga katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na kuanzisha Kanzidata ili kuboresha afya ya mama Wajawazito na huduma ya Watoto wachanga;
- (iii) Kupunguza madhara na vifo mionganoni mwa wagonjwa walioathirika na Virusi

vya UKIMWI kwa kufanya majaribio ya chanjo ya virusi vya UKIMWI na namna ya kuitoa ili iweze kufanya kazi katika kiwango kinachotakiwa;

- (iv) Kupunguza vifo vinavyotokana na Kifua Kikuu kwa kubainisha uwezo wa dawa ya *Isoaniazid* ili kupambana na ugonjwa huo kwa gharama nafuu;
- (v) **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu inaendelea na ukarabati mkubwa wa miundombinu ya majengo ya mihadhara, ofisi, Maabara na Mabweni yanayotumiwa na wanafunzi 4,010 wa fani za Udaktari wa Binadamu, Udaktari wa Magonjwa ya Kinywa na Meno, Ufamasia Uuguzi na Sayansi ya Mazingira katika Chuo Kikuu cha Tiba na Sayansi Shirikishi cha Muhimbili. Aidha, ukarabati wa miundombinu ya maji, ofisi na vyumba vya kufundishia umeendelea katika kituo cha kufundishia cha *Satellite* – Bagamoyo. Kituo hiki hupokea wanafunzi kwa ajili ya mafunzo ya vitendo na utafiti;

Chuo Kikuu cha Ardhi

93. **Mheshimiwa Spika**, Chuo Kikuu cha Ardhi kimefanya tafiti zifuatazo:

- (i) Kujenga miundombinu kwa kutumia

- mchanganyiko wa saruji, mchanga na kemikali maalumu pamoja na kingo za plastiki zinazoweza kutumika mara nyingi bila kuharibika ili kupunguza gharama za ujenzi wa majengo yenye ubora na uimara unaokusudiwa;
- (ii) Kutambua uwezekano wa kutokea majanga ya Bahari katika Bandari ya Tanga kwa kutumia takwimu na taarifa sahihi ili kuwawezesha watumiaji wa Bandari, Wavuvi, Watalii, Watafiti na Watoa Elimu kutoa maamuzi sahihi ya kuepukana na majanga kutohana mabadiliko ya tabia ya bahari; na
 - (iii) Kupunguza athari za milipuko ya volcano ya Mlima Oldonyo Lengai kwa kuweka Vituo vya upimaji vyenye vifaa maalumu vya kuwawezesha Watafiti kupata taarifa sahahi ya hali ya msuguano wa miamba kwa wakati wote ili kutoa tahadhari kwa Wananchi kwa wakati kuepusha madhara.

Chuo Kikuu cha Mzumbe

94. Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Mzumbe kimefanya tafiti zifuatazo:

- (i) Kutathmini matokeo chanya ya kilimo cha mkataba cha miwa ili kimarisha matumizi ya ardhi na kuongeza ajira

- kwa wananchi wanaopakana na mashamba ya miwa nchini;
- (ii) Kutathmini mchango wa kilimo cha mkataba wa zao la tumbaku ili kubainisha manufaa ya bei ya tumbaku katika soko la dunia kwa wakulima wadogo nchini;
- (iii) Kutambua matumizi bora na endelevu ya nishati ili kuzifanya Kampasi za Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki kuwa ni maabara hai za matumizi bora na endelevu ya nishati; na
- (iv) Kubainisha mchango wa mazao ya asali na upasuaji wa mbao ili kuongeza kipato cha Wajasiriamali katika Wilaya ya Mvomero.

USIMAMIZI WA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI

95. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka 2016/17 Wizara yangu imeendelea kusimamia utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali katika Sekta ya Elimu Sayansi na Teknolojia. Miradi na programu hizi zimeiwesha Wizara yangu kuongeza fursa na kuinua ubora wa elimu nchini.

Programu ya Kukuza Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu (KKK)

96. **Mheshimiwa Spika**, Katika juhudi za kuhakikisha kwamba watoto wanaojiunga na Elimu ya Msingi pamoja na walio nje ya mfumo rasmi wanamudu vema stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu, Wizara yangu inaendelea na uratibu wa utekelezaji wa Programu ya Kukuza Stadi za Kusoma Kuandika na Kuhesabu - Programu ya *Literacy and Numeracy Education Support* (LANES). Lengo la programu hii ni kuhakikisha kuwa watoto wanaojiunga na Darasa la I-IV na walio nje ya mfumo rasmi wanajua kusoma kuandika na kuhesabu. Aidha programu hii imewezesha upatikanaji wa vitabu vya kiada na ziada pamoja, nyenzo za kufundishia na uwezeshwaji wa walimu kumudu ufundishaji wa Stadi za Kusoma, Kuandika na Kuhesabu.

Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu II (MMES II)

97. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kutekeleza Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya Pili (MMES II) kwa ushirikiano na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kuanzia mwaka 2010 hadi programu hii ilipofungwa rasmi mwezi Desemba 2016. Katika kipindi cha Julai

2016 Wizara kupitia mradi huu ulifanya yafuatayo: kutoa mafunzo kwa walimu wa sayansi na hisabati, kuandaa kiongozi cha mwalimu kwa masomo ya sayansi kwa wanafunzi wenyewe uono hafifu na kununua vifaa vya kufundishia TEHAMA. Vilevile, Andiko la Programu ya Maendeleo ya Elimu ya Sekondari Awamu ya Tatu (MMES III) lipo katika hatua ya mwisho ya maandalizi.

Programu Lipa Kulingana na Matokeo (Programme for Results - (P4R)

98. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu imeendelea kutekeleza Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo *Programme for Results - P4R* kwa kufadhili Sekta ya Elimu ambapo Serikali hushirikiana na Washirika wa Maendeleo amba ni Benki ya Dunia (World Bank), Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza (Department for International Development - DfID) na Wakala wa Maendeleo ya Kimataifa Sweden (Swedish International Development Agency-SIDA). Programu hii inalenga kujenga uwezo wa Serikali wa kutekeleza vipaumbele vyake ilivyojiwekea na Serikali inapatiwa fedha kutokana na utekelezaji wa vipaumbele hivyo kwa kutumia viashiria vya utekelezaji vilivyokubalika kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kupitia programu hii, Wizara yangu imelipa madeni ya walimu yasiyo

ya mishahara, imekarabati vyuo kumi vya ualimu, imejenga madarasa na kutoa motisha kwa halmashauri.

Mradi wa Kuimarisha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu

99. **Mheshimiwa Spika**, tarehe 24 Machi, 2017 Wizara yangu kwa kushirikiana na Serikali ya Canada imeingia mkataba wa kuboresha Mafunzo na Elimu ya Ualimu unaojulikana kama *Teacher Education Support Project (TESP)*. Mkataba huo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2016/17 – 2020/2021) ambapo kiasi cha **Dola za Canada 53,000,000** sawa na **shilingi bilioni 83** zitatolewa na Serikali ya Canada. Mradi huu utahusisha Vyuo 35 vya Ualimu vinavyofundisha walimu wa Msingi na Sekondari. Lengo kuu la Mradi wa TESP ni kuboresha Mafunzo ya Elimu ya Ualimu inayotolewa katika Vyuo 35 vya Ualimu nchini.

Mradi wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi

100. **Mheshimiwa Spika**, Mradi huu umeandaliwa ili kuwezesha utekelezaji wa Mkakati wa Kitaifa wa Kukuza na Kupanua Stadi za Kazi na Ujuzi. Mkakati huu uliandaliwa na Wizara yangu kwa kushirikiana na Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi Vijana na Ajira, na Watu Wenye Ulemavu. Mradi utajikita katika

kuongeza fursa za upatikanaji wa stadi za kazi na kuongeza ujuzi katika sekta sita za kipaumbele za kukuza uchumi ambazo ni kilimo na kilimo uchumi, utalii, uchukuzi, ujenzi, nishati na madini; na TEHAMA. Uchaguzi wa sekta hizi umezingatia mahitaji makubwa ya waajiri katika sekta hizo; mchango wa sekta katika uchumi; upungufu mkubwa wa wataalamu; uwezo wa kuongeza ajira; na mahusiano kati ya sekta hizi na nyininge.

101. **Mheshimiwa Spika**, lengo kuu la mradi huu wa kukuza ujuzi ni kuimarisha na kupanua upatikanaji na ukuzaji wa stadi za kazi na ujuzi katika ngazi za ufundi na ufundi stadi, Elimu ya Juu na sekta isiyo rasmi kwenye maeneo lengwa. Aidha, mradi unalenga kuimarisha mfumo wa kitaasisi wa kusimamia, kuratibu na kugharimia uendelezaji stadi za kazi katika ngazi ya kitaifa na kisekta kwa kushirikiana na sekta binafsi.

C. **MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2017/18**

102. **Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa Mwaka 2017/18 umezingatia Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (2015-2020), Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 na Ahadi za Viongozi Wakuu wa Serikali. Aidha, imezingatia pia Mpango wa Taifa wa

Maendeleo wa Miaka Mitano wa 2016/17 – 2020/2021, Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (1996), Sera ya Taifa ya Utafiti na Maendeleo (2010), Sera ya Taifa ya Baioteknolojia (2010), Sera ya Taifa ya Teknolojia za Nyuklia (2013) na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

103. **Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka 2017/18 Wizara yangu imepanga kufanya shughuli zifuatazo:

Kuimarisha Mazingira ya Utoaji wa Elimumsingi na Sekondari

104. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu itaendelea kuboresha mazingira ya shule ili kuhakikisha elimu inayotolewa inakidhi ubora unaotakiwa. Katika Mwaka 2017/18 shughuli zifuatazo zitatekelezwa kwa lengo la kuimarisha utoaji elimu:

- (i) kufanya mapitio ya Sheria ya Elimu, Sura 353 pamoja na Sheria za Taasisi zilizo chini ya Wizara ili ziendane na maudhui ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014 kwa lengo la kuimarisha mifumo ya utendaji kazi na kuongeza ufanisi;
- (ii) kukamilisha taratibu za uanzishwaji wa Bodi ya Kitaalamu ya Walimu ambayo ina lengo la kusimamia taaluma ya Walimu hapa nchini.

- (iii) kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo - P4R Wizara itaendelea kuratibu ujenzi wa Vyumba vya Madarasa 2,000 kwa Shule za Msingi na Sekondari na ukarabati wa Shule Kongwe za Sekondari 17, ili kukabiliana na changamoto ya uhaba wa Madarasa na kuwafanya Wanafunzi kujifunza kwa ufanisi zaidi;
- (iv) itagharimia ujenzi na ukarabati wa Miundombinu ya Maji na Vyoo katika Shule za Msingi 1000 na Sekondari 200 kwenye Mikoa ya Dodoma, Mara, Tabora, Mwanza, Kagera, Kigoma, Arusha, Kilimanjaro, Tanga, Simiyu, na Shinyanga kupitia Program ya Huduma ya Maji Elimu ya afya na Usafi wa Mazingira shuleni (SWASH).
- (v) itahakiki shule za sekondari 700 katika mikoa 26 zitakazohusishwa kwenye mradi wa SWASH pamoja na kufanya ufuatiliaji na utoaji ushauri wa ujenzi kwa kutumia miongozo inayotolewa katika ngazi ya halmashauri.
- (vi) itaendelea kusajili Shule za Awali, Msingi, Sekondari na Vituo vinavyotoa Elimu Nje ya Mfumo Rasmi na kutilia mkazo uanzishwaji

wa Shule zenyе mwelekeo wa Sayansi, Kilimo, Teknolojia na Ufundи.

- (vii) itahuisha Miongozo kuhusu ujenzi wa miundombinu ya Shule za Msingi, Sekondari na Vituo vinavyotoa Elimu Nje ya Mfumo Rasmi na kufanya ufuatiliaji katika Shule, Vyuo na Vituo vya Elimu Nje ya Mfumo Rasmi ili kuhakiki uzingatiaji wa masharti ya usajili.

Kuimarisha Utoaji wa Elimu Maalum

105. **Mheshimiwa Spika**, Ili kuongeza fursa za Elimu na Mafunzo kwa Wanafunzi wenyе Mahitaji Maalum kwa Mwaka 2017/18, Wizara yangu itafanya yafuatayo:

- (i) itaimarisha utoaji wa Elimu Maalum na Elimu Jumuishi katika Shule za Msingi na Sekondari kwa kuhuisha miongozo kuhusu miundombinu na vifaa visaidizi kwa wanafunzi wenyе mahitaji maalumu;
- (ii) itapitia utaratibu wa kupima na kutathmini maendeleo ya Wanafunzi wenyе mahitaji maalum kwa lengo la kuongeza ushiriki na ujifunzaji kwa Wanafunzi wenyе mahitaji maalum.
- (iii) itatoa mafunzo kwa Walimu wanaofundisha wanafunzi wenyе

mahitaji maalum wa Darasa la I - IV ambao hawakupata mafunzo katika Mwaka 2016/17. Lengo la mafunzo haya ni kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za KKK na masomo ya Darasa la III hadi la IV kwa kuzingatia Mtaala ulioboreshwa.

Kuimarisha Mafunzo Elimu ya Ualimu

106. Mheshimiwa Spika, Katika kuendeleza na kuimarisha mafunzo ya ualimu, katika mwaka 2017/18 shughuli zifuatazo zitafanyika:

- (i) kuendelea na ujenzi na ukarabati wa Vyuo 6 vya Ualimu vya Kleruu, Mpwapwa, Dakawa, Tabora, Butimba na Marangu. Vilevile, itafanya ukarabati wa miundombinu ya Maktaba na Maabara za TEHAMA katika Vyuo vya Ualimu 35 ili kuweka mazingira rafiki ya kujisomea kwa Wakufunzi na Wanachuo.
- (ii) kuandaa na kuchapisha vitabu na nyenzo muhimu za kujifunzia na kufundishia ili kuwawezesha Wakufunzi na Wanachuo kupata rejea za kutosha na kuwezesha ujifunzaji.
- (iii) itahuisha mitaala ya mafunzo ya Walimu Tarajali katika Vyuo vya Ualimu ili kuendana na mahitaji ya

Mtaala Ulioboreshw na kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa yanalenga kuongeza umahiri na weledi kwa wahitimu.

- (iv) itatoa mafunzo kazini kwa Wakufunzi wa Vyuo vya Ualimu ili kuimarisha uwezo wao katika kumwanda Mwalimu mwenye umahiri na weledi.
- (v) kupitia mradi wa *Tutors Education Program* (TEP) unaofadhiliwa na Serikali ya Canada, Wizara yangu itatoa Mafunzo kwa Wakufunzi wa Hisabati, Sayansi na ICT/TEHAMA (In service Training) kwa Vyuo 35 vya Ualimu ili kuwaongezea ufanisi katika Ufundishaji.
- (vi) itawajengea uwezo Viongozi wa Vyuo vya Ualimu katika uandaaji wa Mpango wa Maendeleo na Uongozi ili kuweza kusimamia vizuri utekelezaji wa mtaala na majukumu ya uendeshaji wa Vyuo.
- (vii) itafanya mapitio ya Mtaala wa Stashahada ya Elimu ya Ualimu ili kupata Mtaala unaokidhi mahitaji ya sasa na kwa kuzingatia pia Mtaala wa Elimu Msingi ulioboreshw.

Kuboresha Mazingira ya Wathibiti Ubora wa Shule

107. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu pia inatambua kuwa Wathibiti ubora wa shule wanakabiliwa na changamoto ya kutokuwa na mazingira wezeshi ya kufanya kazi zao kwa ufanisi. Hivyo, katika mwaka 2017/18 Wizara itajenga Ofisi 50 za Uthibiti Ubora wa Shule za Wilaya. Ujenzi wa Ofisi hizi utazingatia Wilaya ambazo zipo katika Majengo ya kupanga, Wilaya mpya ambazo hazina Ofisi na Wilaya ambazo tayari zimetenga maeneo ya ujenzi. Ujenzi wa Ofisi hizo utaboresha mazingira ya kufanyia kazi, kupunguza gharama za kulipia pango na kuelekeza fedha hizo kwenye shughuli nahsusini zinazolenga kuthibiti ubora wa shule.
108. **Mheshimiwa Spika**, Sambamba na ujenzi wa ofisi, katika Mwaka 2017/18, Wizara yangu imepanga pia kufanya yafuatayo katika eneo la la Uthibiti Ubora ya Shule:
- (i) itakagua Ubora wa Elimu katika Shule 11,021 zikiwemo Shule za Msingi 8,513, Sekondari 2,375, Vyuo vya Ualimu 133 na Vituo vinavyotoa Elimu ya Watu Wazima na Vituo vya Elimu Nje ya Mfumo Rasmi na kutoa ushauri wa kitaalamu na kitaaluma kwa Walimu kwa lengo la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji.

- (ii) itaboresha mazingira ya kufanya kazi kwa kuongeza vitendea kazi katika Ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule katika wilaya 20 na Kanda 11. Vifaa vitakavyonunuliwa ni pamoja na Kompyuta 100, *Photocopy Machine* 31, *Printer* 31 na *Scana* 31 na Samani za Ofisi.
- (iii) itafungua ofisi za Uthibiti Ubora wa Shule katika baadhi Wilaya mpya za Ubungo, Kigamboni, Chalinze, Nanyamba, Uvinza, Kakonko, Butiama, Ushetu, Msalala na Mlele ili kusogeza huduma za Uthibiti Ubora wa Shule karibu na Wadau. Vigezo vilivyotumika kuchagua Wilaya hizo ni kutokana na idadi ya Shule zilizopo katika Wilaya zilizoanzishwa, umbali kutoka ofisi ya Uthibiti Ubora wa Shule ya Wilaya ya jirani (Wilaya mama) na utayari wa Wakurugenzi wa Halmashauri husika katika kusaidia uanzishaji wa ofisi.
- (iv) itaendelea kufanya ufuatiliaji na tathimini ya utekelezaji wa Sera, Nyaraka na Miongozo kuhusu uboreshaji wa Elimumsingi na Sekondari, pamoja na kufanya tafiti kwa lengo la kubaini changamoto zinazojitokeza katika utoaji wa

Elimumsingi na Sekondari na kuzipatia ufumbuzi.

- (v) itafanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Elimu ya Mwaka 2014 na kutumia mapendekezo yake katika kuimarisha utendaji kazi katika ngazi mbalimbali.

Mradi wa Elimu na Kukuza Stadi za Kazi na Ujuzi (ESPJ)

109. **Mheshimiwa Spika**, Wizara yangu kupitia Mradi wa Elimu na kukuza stadi za kazi na ujuzi itatekeleza yafuatayo katika mwaka 2017/18:

- (i) Kuandaa Mwongozo wa Utekelezaji kwa kuhusisha Wadau;
- (ii) Kukamilisha uundwaji wa Baraza la Kitaifa la kuendeleza na kusimamia Stadi za Kazi;
- (iii) Kutengeneza Mfumo wa namna ya kuunda na kutumia *Student Voucher Scheme* kwa kushirikiana na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu pamoja na Wadau;
- (iv) Kuandaa Mfumo Huishi wa Taarifa (*online information system*) kuhusu Utoaji wa Elimu na Mafunzo katika

Vyuo na Taasisi zote za Elimu na Mafunzo kwa kushirikiana na TCU na NACTE, na VETA; na

- (v) Kujenga uwezo wa Taasisi zinazosimamia na kuratibu Elimu ya Juu na Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini.

Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo

110. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/18, Wizara yangu kupitia Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo itaendelea kuratibu utoaji wa motisha kwa Halmashauri zote pamoja na kufanya Ufutiliaji na Tathmini ya Uendeshaji wa Shule ili kuimarisha ubora wa utoaji elimu nchini. Vilevile Wizara itanunua Vifaa vya Maabara Awamu ya Pili ambapo awamu ya mwisho inategemewa kukamilika mwaka 2018/19. Wizara pia itasomesha Wahadhiri 100 katika Shahada ya Uzamivu kwenye fani zilizo na uhaba mkubwa wa wahadhiri katika Vyuo Vikuu vya Umma ili kuhakikisha elimu inayotolewa nchini ina ubora unaotakiwa. Aidha, shule ya kisasa ya Sekondari itajengwa katika mkoa wa Dodoma kwa lengo la kuongeza miundombinu ya elimu katika makao makuu ya nchi.

URATIBU WA TAASISI NA WAKALA ZILIZO CHINI YA WIZARA

111. **Mheshimiwa Spika**, Wizara itaendelea kuratibu shughuli za Taasisi na Wakala tunazozisimamia. Shughuli zilizopangwa kufanyika mwaka 2017/18 katika Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni kama ifuatavyo:

Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania

112. **Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka 2017/18, Bodi ya Huduma za Maktaba Tanzania itafanya yafuatayo:

- (i) itaendeleza na kuboresha huduma za maktaba kwa kujenga maktaba ya Chuo cha Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka cha Bagamoyo (*SLADS*),
- (ii) itafanya upanuzi na ukarabati wa jengo la Maktaba ya Dodoma pamoja na ukarabati wa majengo ya Maktaba za Mikoa ya Tabora, Rukwa na Mwanza; na
- (iii) itaanza ujenzi wa Maktaba za Mikoa ya Singida na Shinyanga ili kutoa fursa kwa Wananchi wa Mikoa hiyo kupata huduma za Maktaba.
- (iv) itaongeza machapisho/vitabu 40,000 kwa ajili ya watu wazima na watoto pamoja na kuboresha upatikanaji wa

vifaa vya TEHAMA ili kuongeza ari ya usomaji katika jamii.

- (v) itaendelea kutoa ushauri wa kitaalam juu ya uanzishaji na uendeshaji wa Maktaba za Shule, Vyuo, Taasisi na Halmashauri za Miji, Manispaa na Wilaya nchini; na
- (vi) itatoa mafunzo ya Ukutubi na Uhifadhi Nyaraka kwa wafanyakazi wa Maktaba katika Ngazi ya cheti na Diploma.

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima Tanzania (TEWW)

113. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/18 Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima itatekeleza yafuatayo:

- (i) Kuandaa mkakati wa kusaidia kupunguza idadi ya wasiojua kusoma na kuandika kwa kuandaa mafunzo ya wawezeshaji wa programu za kisomo na kufanya kampeni ya Kisomo (Literacy Programmes);
- (ii) Kuongeza udahili wa wanafunzi katika programu mbalimbali wakiwemo vijana na watu wazima wanaopata Elimu ya sekondari nje ya mfumo rasmi kutoka 18,675 mpaka 20,000 na wanafunzi 1,500 wa programu za astashahada na stashahada;

- (iii) Kuboresha programu za mafunzo kwa kudurusu mitaala;
- (iv) Kujenga na kukarabati majengo katika mikoa ya Rukwa (uzio), Morogoro WAMO (Maktaba na Vyoo), Kilimanjaro (ukarabati), Kagera (Ofisi) na Dar es Salaam (Library Extension);
- (v) Kuimarisha uwezo wa Maktaba ya TEWW kwa kununua na kuweka vitabu 1,000 vya kiada na ziada na kutumia TEHAMA katika usomaji; na
- (vi) Kujenga na kuweka mtandao wa TEHAMA (Local Area Network - LAN) ili kuimarisha miundombinu ya ufundishaji na ujifunzaji.

Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM)

114. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2017 / 18, Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu utafanya shughuli zifuatazo:

- (i) Ukarabati wa jengo la zamani na mabweni 3 ya Wanafunzi na kuanza ujenzi wa ukumbi wa mihadhara katika Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu Kampasi ya Bagamoyo na kuanza ujenzi katika vituo vya Mwanza na Mbeya;

- (ii) Itafanya Tafiti 4 za kielimu kuhusu uendeshaji na Usimamizi bora wa taasisi za kielimu na kutoa Ushauri Elekezi juu ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu nchini. Tafiti 4 zitakazofanyika zitahusu utafiti kuhusu ufanisi wa mafunzo ya KKK yaliyotolewa kwa walimu wanaofundisha madarasa ya awali; athari za mafunzo ya Cheti cha Uongozi na Usimamizi wa Elimu katika kuimarisha utendaji kazi wa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi katika Mikoa ya Njombe, Mbeya, Songwe na Iringa; ufanisi wa mrejesho kutoka kwa Wathibiti Ubora, katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji katika Elimu Msingi na tathmini ya maandalizi ya kupambana na majanga katika Taasisi za kielimu.
- (iii) Itatoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi wa Elimu kwa viongozi 1,500 wa idara mbalimbali za Elimu; mafunzo ya Stashahada ya Ukaguzi wa Shule kwa Wakaguzi 1,000 kutoka katika Wilaya zote za Tanzania Bara; na mafunzo ya cheti cha Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi 706 kutoka katika Mikoa ya Iringa, Mbeya na Njombe;

- (iv) Itatoa mafunzo ya muda mfupi ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Wajumbe 10,000 wa Bodi za Shule za Sekondari kuhusu mbinu bora za usimamizi wa Elimu ya Sekondari katika Shule; na mafunzo ya awali ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Wakuu wapya wa Shule za Sekondari 1,500 kutoka katika Mikoa yote ya Tanzania Bara; na
- (v) Itatoa Mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu kwa Wakuu 300 wa Shule za Sekondari zisizo za Serikali, Mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu na Stadi za KKK kwa Wathibiti Ubora wa Shule 1,400, mafunzo ya Uongozi na Uendeshaji wa Elimu na Stadi za KKK kwa Maafisa Elimu 528 na mafunzo kwa Walimu 45,000 wa Darasa la I na II kuhusu Stadi za KKK kwa Mikoa ya Tanzania Bara.

Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi (FDC)

115. Mheshimiwa Spika, Mwaka 2016 usimamizi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ulihamishiwa katika Wizara yangu. Kwa kuzingatia hali halisi ya vyuo hivyo, Wizara itaboresha hatua kwa hatua mazingira yake ya kujifunzia na

- kufundishia ili kuhakikisha kuwa vinatoa mafunzo yanayokidhi mahitaji ya sasa.
116. Katika mwaka 2017/18 Wizara itafanya yafuatayo:
- (i) itaendelea kuchambua hali halisi ya Rasilimali zilizopo katika Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi ikiwemo Wakufunzi, Watumishi wasio Wakufunzi, Miundombinu, Vifaa vya kujifunzia na kufundishia kwa lengo la kubaini mahitaji halisi na kuweka mpango wa muda mrefu wa uboreshaji wa vyuo hivyo.
 - (ii) itakarabati na kuboresha miundombinu ya Vyuo 10 vya Maendeleo ya Wananchi ili kuweka mazingira bora ya kutolea Mafunzo ya Ufundi Stadi na kuongeza udahili.
 - (iii) itawajengea uwezo Wakufunzi wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na mrefu ili waweze kutoa elimu bora ya nadharia na vitendo kwa wanafunzi.
 - (iv) itaendelea kuvipatia Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi Vifaa, Mitambo na Mashine za kisasa za kufundishia na kujifunzia ili viweze kutoa elimu na mafunzo bora kwa walengwa.

- (v) Itafuatialia upimaji maeneo ya Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi kuviwezesha kupata Hati Miliki ya Ardhi. Hatua hii inalenga kuondoa changamoto ya uvamizi wa ardhi katika Vyuo hivyo.

Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi

117. Mheshimiwa Spika, Katika Mwaka 2017/18, NACTE itafanya yafuatayo:

- (i) Itaendesha mafunzo kwa Maofisa Udhili katika Taasisi na Vyuo kuhusu namna ambavyo vinaweza kusaidia wanafunzi kufanya udhili;
- (ii) itakagua na kusajili Vyuo 50 vyenye sifa ya kutoa Mafunzo ya Elimu ya Ufundi, kukagua na kutoa miongozo itakayoviwezesha Vyuo 100 kupata ithibati kwa kuzingatia vigezo vilivyowekwa. Aidha, itafuatialia na kutathmini Vyuo 350 vya Elimu ya Ufundi ili kuhakikisha mafunzo yanayotolewa ni yenye ubora na yanakidhi mahitaji ya soko la ajira. Vilevile, itaratibu utengenezaji wa Mitaala 45, kuhuisha Mitaala 10 na kuhakiki Mitaala 50 inayozingatia umahiri katika Vyuo vya Elimu na Ufundi nchini ili kukidhi mahitaji ya soko la ajira;

- (iii) itaendelea kutengeneza na kuboresha Mifumo ya Kieletroniki itayosaidia kuhakikisha ubora wa Elimu ya Ufundı ikiwemo Mifumo ya ukusanyaji wa Takwimu za Wanafunzi; usimamizi wa Rasilimali watu Vyuoni na Mfumo wa Kutoa Vyeti na *transcript* kwa Wanafunzi wa Vyuuo vya Elimu ya Ufundı.

Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı Stadi - VETA

118. **Mheshimiwa Spika**, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı Stadi (Vocational Education and Training Authority) ilianzishwa mwaka 1994 kwa Sheria ya Bunge Sura ya 82 kwa lengo la kutoa mafunzo ya ufundı stadi na kusimamia ithibati na uthibiti wa mafunzo ya ufundı stadi nchini.
119. Katika mwaka wa fedha wa 2017/18 Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundı Stadi (VETA) imepanga kutimiza malengo yafuayayo:-
- (i) itaendelea kufuatilia ujenzi wa Vyuuo vya Ufundı Stadi vya Mikoa ya Njombe, Geita, Simiyu na Rukwa;
 - (ii) itaanza ujenzi wa Chuo cha Ufundı Stadi cha Mkoa wa Kagera ambao umechelewa kuanza kutokana na

- kutokuwepo kwa miundombinu muhimu kama vile umeme na barabara inayofikika kwa urahisi katika eneo lililotengwa. Mamlaka husika zinafanya kazi suala la miundombinu na ujenzi wa Chuo utaanza mara baada ya ufumbuzi wa changamoto hizo kupatikana;
- (iii) itakamilisha ujenzi wa Chuo cha Ufundı Stadi cha Wilaya ya Namtumbo pamoja na ukarabati wa Chuo cha Ufundı Stadi cha Wilaya Karagwe;
 - (iv) itaanza ujenzi wa Vyuo vya Ufundı Stadi katika Wilaya za Chato, Chunya, Kilindi, Nyasa na Ukerewe pamoja na ujenzi wa Karakana ya Mitambo ya Kilimo na Vyumba vinne (4) vya Madarasa katika Chuo cha Ufundı Stadi cha Mkoa wa Arusha kilichopo Oljoro;
 - (v) itakamilisha ujenzi wa Karakana za Useremala, Umeme wa Magari na Jengo la Utawala katika Chuo cha Mkoa Morogoro-Kihonda; pamoja na kukamilisha ujenzi wa Karakana kumi na moja (11) za Vyuo vya Ufundı Stadi vya Mikoa ya Lindi (4), Pwani (3), na Manyara (4);

- (vi) itajenga mabweni mawili katika Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro;
- (vii) itanunua vifaa vyaa kufundishia na kujifunzia katika Chuo cha Ualimu wa Ufundi Stadi Morogoro na kununua vitabu vyaa kiada na ziada kwa Vituo 7 vyaa Kanda za Vyuo vyaa Ualimu;
- (viii) itasimamia mafunzo ya ufundu stadi nchini na kuendelea na usajili wa Vyuo na kutoa Ithibati na Uthibiti wa Mafunzo ya Ufundu Stadi nchini;
- (ix) itaendesha mafunzo na kusimamia mafunzo ya ufundu stadi ya muda mrefu na muda mfupi katika Vyuo vyaa Ufundu Stadi 761 nchini vikiwemo 29 vinavyomilikiwa na VETA na kusimamia utoaji wa mafunzo ya Ualimu wa Ufundu Stadi katika Chuo cha Walimu wa Ufundu Stadi Morogoro (MVTTC) kwa Walimu 700;
- (x) itawezesha mafundi 8,320 kutoka sekta isiyo rasmi kutambuliwa na kurasimishwa baada ya kufanyiwa tathmini (Recognition of Prior Learning) katika fani mbalimbali kwa kushirikiana na wadau ikiwemo ofisi ya Waziri Mkuu-Kazi, Vijana, Ajira na Watu Wenye Ulemavu;

- (xi) itawajengea uwezo wa kufanya kazi kwa vitendo wahitimu wa ufundi stadi katika vituo atamizi vyta wahitimu (*incubators*);
- (xii) itaongeza wigo wa waajiri wanaotoa mafunzo ya Uanagenzi (*Apprenticeship*) na kuboresha stadi za kazi/ujuzi kwa Wajasiriamali 3,000 kupitia Programu ya *Integrated Training for Entrepreneurship Promotion – INTEP*.

Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania

120. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (Tanzania Commission for Universities-TCU) ni Taasisi ya Serikali iliyoundwa mwaka 2005 chini ya Sheria ya Vyuo Vikuu Sura ya 346 ya Sheria za Tanzania, kufuatia maboresho yaliyofanywa na Serikali kwa lililokuwa Baraza la Ithibati la Elimu ya Juu (HEAC) lililoanzishwa kwa Sheria ya Elimu Sura ya 523 ya Sheria za Tanzania.
121. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/18, Tume ya Vyuo Vikuu itafanya kazi zifuatazo:
- (i) itaendelea kusimamia ubora wa Elimu ya Juu kwa Kupitia Mifumo na Miongozo mbalimbali inayotumika kusimamia Uthibiti na Ithibati ya Elimu ya Juu nchini na Kukagua

Vyuo 25 vya Elimu ya Juu kwa lengo la kuhakiki ubora wake.

- (ii) itafanya tathmini kwa programu 100 za masomo katika Vyuo Vikuu nchini na Kufanya tathmini na kutambua Tuzo 3,000 za ngazi za Shahada zilizotolewa katika Vyuo vya Elimu ya Juu nchi za nje;
- (iii) itaanzisha Mfumo wa kutumia TEHAMA katika ukusanyaji taarifa kutoka vyuo vya Elimu ya Juu nchini ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa kwa wakati kwa ajili ya mipango na maamuzi ya kisera na kiutendaji; na
- (iv) Itashiriki katika makongamano na mikutano ihusuyo uimarishaji na Uthibiti wa Ubora wa Elimu ya Juu katika ukanda wa Afrika Mashariki na kimataifa kwa lengo la kuongeza ujuzi na weledi katika kuthibiti ubora wa elimu ya juu nchini.

Chuo cha Ufundı Arusha

122. Mheshimiwa Spika, Chuo Chuo cha Ufundı Arusha (ATC) kilianzishwa mwaka 1978 kwa lengo la kutoa mafunzo ya ufundı sanifu katika fani mbalimbali za elimu ya ufundı. Mwaka 2007 Chuo kilianza kujitegemea kiutendaji (Autonomous Institution) kupitia Tamko (Establishment Order) Namba 78 chini ya sheria ya Bunge

namba 9 ya mwaka 1997 ya Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE). Katika mwaka 2017/2018 Chuo Cha Ufundi Arusha (ATC) kitatekeleza yafuatayo:

- (i) Kudahili wanafunzi 1,065 wa mwaka wa kwanza, Astashahada (55), Stashahada (800) na Shahada (210);
- (ii) Kuanzisha program mpya za stashahada katika fani mbalimbali za kiufundi na teknolojia kwa kuzingatia sera za kitaifa na mahitaji ya soko ambazo ni pamoja na “Pipe Works, Oil and Gas Engineering” na “Electrical and Hydropower Engineering”;
- (iii) Kujenga Jengo la Madarasa na Maabara kwa fani za Madini na Vito, Uhandisi wa Vifaa Tiba, Uhandisi wa Mawasiliano ya Anga na Teknolojia ya Mawasiliano ya Habari;
- (iv) Kukarabati na kununua vifaa vyakaraka za Useremala, Uhandisi Magari na Uhandisi Mitambo;
- (v) Kuboresha elimu ya ufundi kwa kugharimia mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa wafanyakazi (wanataaluma 15 na waendeshaji 10) na kuajiri wafanyakazi wapya 104 (waendeshaji 22 na wanataaluma 82);
- (vi) Kuhuisha mitaala 12 ya programu zilizopo za Ufundi Sanifu (NTA 4-6);

- (vii) Kutekeleza Mpango Mkakati wa kuanzisha Mafunzo ya Umeme utokanao na nishati ya maji na uundaji wa mitambo midogo ya kuzalisha umeme utokanao na nishati ya Maji na kufufua kituo cha uzalishaji umeme cha Kikuletwa;
- (viii) Kuendeleza shamba la mafunzo ya kilimo na umwagiliaji la Oljoro;
- (ix) Kuendeleza ushirikiano na nchi wahisani, mashirika ya kimataifa, Vyuo vya Elimu ya Juu na vya Ufundii vilivyo nchini na vya kimataifa;
- (x) Kuendelea na utafiti wa kupima uimara wa udongo, kokoto na lami zinazotumika katika ujenzi wa barabara ili kuanisha ubora wake na kutoa ushauri wa matumizi sahihi wakati wa ujenzi wa barabara na pia kuongeza umahiri wa mafundi sanifu kwenye ujenzi wa barabara;
- (xi) Kuendelea kuboresha fimbo inayowasidia walemvu wa macho electronic blind stick katika kutambua sehemu za mapitio yao ili kuwaongoza kwa urahisi. Hii itasaidia upatikanaji nwa fimbo hizo kwa gharama nafuu;
- (xii) Kitaendelea kuunda Helikopta ya gharama nafuu na salama kwa safari fupi nchini ili kurahisisha usafiri katika maeneo yasiyofikika kwa

- usafiri wa gari kwa urahisi; na
- (xiii) Kitaboresha Mafunzo kwa kununua mashine na mitambo ya kisasa, kwa fedha zilizotolewa na Serikali ya Austria kama mkopo wa masharti nafuu wa **Euro 6,000** sawa na takriban shs **billionsi 14**. Aidha, Chuo kitaimarisha ufundishaji na kutoa mafunzo yenye lengo la kujenga uwezo kwa wanataaluma ili waweze kutumia mitambo ya kisasa itakayonunuliwa.

Baraza la Mitihani la Tanzania

123. **Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka 2017/18, Wizara yangu kupitia Baraza la Mitihani imepanga kutekeleza yafuatayo:

- (i) Kuendesha Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi kwa watahiniwa 900,000 wanaotarajiwa kufanya mtihani huo Septemba, 2017;
- (ii) Kuendesha Upimaji wa Kitaifa wa Darasa la Nne kwa watahiniwa 1,060,000 wanaotarajiwa kufanya upimaji huo Novemba, 2017;
- (iii) Kuendesha upimaji wa Kitaifa wa kidato cha Pili kwa watahiniwa 450,000 wanaotarajiwa kufanya upimaji huo mwezi Novemba, 2017;
- (iv) Kuendesha Mtihani wa Kidato cha

- Nne kwa watahiniwa 440,000 na wa mtihani wa Maarifa kwa watahiniwa 15,000 wanaotarajiwa kufanya mitihani hiyo Novemba, 2017;
- (v) Kuendesha Mtihani wa Kidato cha Sita kwa watahiniwa 73,000 wanaotarajiwa kufanya Mtihani huo Mei, 2018; na
 - (vi) Kuendesha Mtihani wa Cheti na Diploma ya Ualimu wa marudio kwa watahiniwa 5,000 wanaotarajiwa kufanya Mtihani huo Mei, 2018.

Taasisi ya Elimu Tanzania

124. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/18, Wizara kupitia Taasisi ya Elimu Tanzania imepanga kutekeleza yafuatayo:

- (i) Kuchapa vitabu vya Kiada kwa Darasa la IV na Masomo ya Elimu ya Sekondari kwa Kidato cha I-VI;
- (ii) Kutathmini machapisho mbalimbali yaliyoandikwa na makampuni/watu binafsi ikiwemo yale yaliyo katika mfumo wa kielektroni;
- (iii) Kuboresha Mtaala wa Elimu ya Ualimu na kuandaa moduli zake;
- (iv) Kuratibu na kuendesha programu

za ufundishaji na ujifunzaji kwa kutumia TEHAMA; na

- (v) Kuendesha mafunzo kazini kwa Walimu wa Elimumsingi na Sekondari ili kuboresha utendaji kazi wao.

Tume ya Taifa ya UNESCO

125. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/18, Tume ya Taifa ya UNESCO imepanga kutekeleza yafuatayo:

- (i) Kuratibu mafunzo kwa ufadhilli wa UNESCO; na kuandaa Mikutano kwa ajili ya kuwajengea uwezo vijana ili kutekeleza shughuli za UNESCO kwa kujenga uelewa wa Malengo endelevu; na
- (ii) Kuandaa maandiko matano ya Miradi ya kuboresha elimu kwa ajili ya ufadhilli kutoka UNESCO na Wadau wengine; na kuandaa Jarida la Tanzania na UNESCO Toleo namba 14.

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

126. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/18, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu imepanga kutekeleza yafuatayo:

- i. Kutoa Mikopo na Ruzuku kwa

wanafunzi wanufaika na mikopo.

- ii. Kuboresha vigezo vyatambuzi ili kuwawezesha Wanafunzi wasio na uwezo wa kiuchumi kupata Elimu ya Juu kuititia Mikopo na Ruzuku;
- iii. Kupunguza utegemezi wa kifedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali kwa asilimia 35%; na
- iv. Kutambua vyanzo vingine vyakuchangia Mfuko wa Mikopo ya Elimu ya Juu na Ufundi kwa ajili ya kukopesha wanufaika wengi.

Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia

- 127. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia itaendelea kuratibu maandiko yatokanayo na tafiti mbalimbali *Policy Briefs* katika Taasisi za utafiti ili kuwawezesha maamuzi kufanyika kwa kutumia ushahidi wa kisayansi.
- 128. Katika mwaka 2017/18 itafanya shughuli zifuatazo:
 - (i) itafadhili miradi mipyaa na inayoendelea ya utafiti katika maeneo ya Viwanda, TEHAMA, Kilimo, Afya, Mazingira na Maliasili.
 - (ii) Wafadhili watafiti kutoka Taasisi

za utafiti za umma wataendelea kuwezeshwa kusoma shahada za uzamivu katika vyuo vyao ndani ya nchi.

- (iii) itaendelea kuimarisha matumizi ya matokeo ya utafiti na ubunifu kutoka taasisi za ndani ya nchi ili yaweze kuleta manufaa ya kibiashara.

Chuo Kikuu cha Dar es Salaam

129. **Mheshimiwa Spika**, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD) ni Chuo Kikuu cha umma ambacho kilianzishwa rasmi tarehe 1 Julai, 1970 na kupata ithibati ya Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU), Namba 005, mnamo tarehe 24 Novemba, 2006.
130. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/18 kitatekeleza yafuatayo:
- (i) Kuongeza idadi ya wanafunzi wa shahada za awali kutoka 24,182 hadi 25900 (ongezeko la asilimia 7). Wanafunzi wa shahada na stashahada za uzamili wataongezeka kutoka 2092 hadi 2510 (ongezeko la silimia 20) na wa stashahada na astashahada wataongezeka kutoka kutoka 182 hadi 218 (ongezeko la asilimia 20).
 - (ii) Kuongeza idadi ya miradi ya utafiti, hasa yenye ufadhili wa washirika wetu wa maendeleo ambapo maandiko ya

- miradi yamewasilishwa na mengine yanaendelea kutayarishwa;
- (iii) Kuongeza idadi ya majarida ya kimataifa ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kutoka 5 kwa sasa hadi 21 na kuyafanya yafikike kwa njia ya mtandao;
 - (iv) Kupanua wigo wa “Juma la Utafiti” na kuonyesha matokeo ya tafiti za Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kupitia runinga na redio;
 - (v) Kutoa mafunzo maalum ya utafiti na uchapishaji kwa wanataluma 100 na wanafunzi 100 wa shahada za uzamili;
 - (vi) Kuanzisha kituochakuatamiaubunifu mpya (incubator) kitakacho jumuisha maeneo mbalimbali ya kitaaluma.
 - (vii) Kutoa mafunzo maalum ya ushauri wa kitaalam kwa wanataluma 100 na wafanyakazi 50 wa kada nyinginezo. Pia kutoa mafunzo ya kisasa kwa jamii, ya muda mfupi na wa kati, katika nyanja mbalimbali na teknolojia mpya na za kisasa; na
 - (viii) Kupanua wigo wa kutangaza huduma za ushauri kwa njia mbalimbali, kama kushiriki maonesho ya kitaifa na kimataifa na/au kutumia runinga,

- magazeti, machapisho na vipeperushi.
- (ix) Kukarabati bweni Na. 5 la Kampasi ya Mwl. J.K. Nyerere Mlimani na kufanya ukarabati wa miundombinu ya maji safi na maji taka;
- (x) Ujenzi wa awamu ya pili ya Kituo cha Buyu (Zanzibar) kwa ajili ya Taasisi ya Sayansi za Bahari; Kujenga ofisi mpya ya michezo katika viwanja vyatya michezo vya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Kuongeza ghorofa mbili na samani katika mabweni mapya yanayojengwa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kwa ufadhili wa Serikali; na sehemu ya gharama za kujenga miundombinu na kununua vifaa kwa ajili ya hospitali maalum ya mafunzo ya udaktari bingwa;
- (xi) kununua samani na vifaa vya maabara kwa ajili ya majengo mapya na kufanya ununuzi wa vitabu na mashubaka kwa ajili ya Maktaba mpya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam; na
- (xii) Kuongeza Vifaa tiba katika Kituo cha Afya cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kufanya matengenezo viwanja na kuongeza vifaa vya michezo.

Chuo Kikuu cha Dodoma

- 131. Mheshimiwa Spika,** Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) ni Chuo cha umma kilichoanzishwa baada ya kutiwa saini kwa Hati Idhini ya Chuo tarehe 5 Machi, 2007 na kwa kuzingatia sheria ya vyuo vikuu Namba 7 ya mwaka 2005.
- 132. Mheshimiwa Spika,** Malengo ya Chuo kwa mwaka 2017/2018 ni haya yafuatayo;
 - (i) Kudahili wanafunzi wapya 8,412 wa shahada ya kwanza, Kudahili wanafunzi wapya 3,124 wa Stashahada na Astashahada, Kudahili wanafunzi wapya 348 wa shahada za Uzamili na Uzamivu. Chuo kina lengo la kuwa na jumla ya wanafunzi 28,367 kwa mwaka wa masomo 2017/2018;
 - (ii) Kuanza ujenzi wa Ukumbi mmoja wa Mihadhara katika Chuo cha Sayansi Asilia na Hisabati; Ujenzi wa Ukumbi mmoja wa Mihadhara katika Chuo cha Sayansi za Ardhi; na Ujenzi wa Madarasa na Ofisi katika Chuo cha Sayansi Asilia na Hisabati pamoja na Chuo cha Sayansi za Ardhi;

- (iii) Kuanza Ujenzi wa Awamu ya pili Chuo cha Sayansi za Afya; Pamoja na Ujenzi wa nyumba 100 za Wafanyakazi Awamu ya Kwanza (nyumba nane (8) za ghorofa kwa ajili ya familia nane kila moja – 64 na nyumba 36 kwa ajili ya Viongozi ikiwa ni pamoja na Makamu Mkuu wa Chuo, Manaibu Makamu Wakuu wa Chuo, Wakuu wa Vyuo, Wakurugenzi na Wakuu wa Skuli;
- (iv) Ununuzi wa magari 20; Ununuzi wa kompyuta; Ununuzi wa vifaa vya maabara; na
- (v) Ununuzi wa Samani za Ofisi, Makazi, Madarasa, Maabara na Mabweni ya wanafunzi; na Ukarabati wa Mabweni, Madarasa na majengo mengine ya Chuo;
- (vi) Kununua vifaa muhimu vya kufundishia pamoja na zana za kufundishia;
- (vii) Kuwapeleka masomoni wafanyakazi 268. Kati ya hao 177 ni watakao kwenda kuanza masomo na 91 ni wafanyakazi wanaoendelea na masomo (shahada ya Uzamivu 81, shahada ya Uzamili 86, Shahada za Awali 15, Stashahada 23,

- Astashahada 14, mafunzo ya muda mfupi 32, na watakaosomeshwa nje ya nchi 17); na
- (viii) kuajiri wafanyakazi wapya 445 ili kukidhi ikama ya wafanyakazi.

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo

133. **Mheshimiwa Spika**, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kilianzishwa tarehe 1 Julai, 1984 chini ya Sheria Na.6 ya mwaka 1984 iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 11 Aprili, 1984 na kurekebishwa na Sheria Na.14 ya mwaka 1984. Sheria hiyo ilifutwa kwa Sheria namba 7 ya mwaka 2005 ya Vyuo Vikuu ambayo ilikipa Chuo mamlaka ya kuwa na Hati idhini yake ya mwaka 2007.
134. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka 2017/18 Chuo kitatekeleza yafuatayo:
- (i) Kuanzisha shahada mpya za kwanza sita (6) na shahada za uzamili tisa (9) na masomo yasiyo ya shahada katika fani nne (4) ili kuendana na mahitaji ya soko la ajira; na
 - (ii) Kuongeza udahili wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza wakiwemo wanafunzi wa shahada za kwanza kutoka 3,004 hadi 4,456, shahada za juu (Uzamili na Uzamivu) kutoka 166;

- (iii) kufanya tafiti mbalimbali zaidi ya 150 katika kulenga uboreshaji na uzalishaji wa mzao ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi n.k ili kupunguza umaskini kwa Wananchi.
- (iv) Kuongeza utoaji wa Elimu na Ushauri kwa wakulima kwa kutumia mbinu mbalimbali kama semina, kozi fupi, warsha, luninga na radio;
- (v) Kuendesha programu 80 za utoaji wa Elimu na Ushauri wa kitaalamu kwa washiriki 350 wakiwemo Wakulima, Maafisa Ugani na Watafiti;
- (vi) Kukarabati vyumba 6 vya mihadhara vilivyomo Kampasi ya Solomon Mahlangu pamoja na Kumbi na Hosteli za Taasisi ya Elimu ya Kuijendeleza;
- (vii) Kuendelea kuboresha nyumba za wafanyakazi kwa kukarabati nyumba 60;
- (viii) Kuendelea kuboresha mabweni ya wanafunzi kwa kukarabati mabweni 4;
- (ix) Kuboresha mazingira ya kufundishia na kusomea ikiwa ni pamoja na kuongeza kiwango cha upatikanaji wa vifaa na zana za kufundishia;
- (x) Kukamilisha miradi ambayo inaendelea ikiwepo Mradi wa Ujenzi wa Maabara katika Kampasi ya

Solomon Mahlangu;

- (xi) Kuongeza miundombinu mipyä ya kufundishia ambayo ni pamoja na ujenzi wa Ukumbi wa Mihadhara, Ujenzi wa Maabara, Ujenzi wa Viti vya Kusomea na Hosteli moja ya wanafunzi wa Uzamili na Jengo la Ofisi za Wafanyakazi; na
- (xii) Kuendelea kujenga mahusiano na Taasisi nyingine ndani na nje ya nchi.

Chuo Kikuu Mzumbe

- 135. **Mheshimiwa Spika**, Chuo Kikuu Mzumbe kilianzishwa kwa Sheria ya Chuo Kikuu Mzumbe Na. 9 ya mwaka 2001. Kwa sasa, Chuo kinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Hati idhini ya Chuo ya mwaka 2007 iliyotolewa chini ya Kifungu cha 25 cha Sheria ya Vyuo Vikuu ya Mwaka 2005.
- 136. **Mheshimiwa Spika**, Chuo Kikuu Mzumbe kwa mwaka 2017/18 kimepanga kutekeleza yafuatayo;
 - (i) Kudahili wanafunzi wapya 5,092 katika programu mbalimbali (astashahada - 250, stashahada - 200, shahada ya kwanza - 3,463, shahada ya umahiri - 1,174 na shahada ya uzamivu - 5).
 - (ii) Kukamilisha utafiti katika maeneo 41 na kutoa ushauri wa kitaalamu katika maeneo 50 ya menejimenti,

- uongozi, teknolojia na sayansi ya jamii kwa ujumla.
- (iii) Kukarabati mabweni nane (8) ya wanafunzi Kampasi Kuu Mzumbe;
 - (iv) Kukarabati ofisi za watumishi Kampasi ya Dar es Salaam;
 - (v) Kukarabati na kujenga miundombinu ya Kampasi ya Mbeya;
 - (vi) Kujenga kumbi mbili (2) za miadhara Kampasi Kuu Mzumbe;
 - (vii) Kujenga jengo la kitaaluma kwa ajili ya programu za Sayansi na Teknolojia Kampasi Kuu Mzumbe;
 - (viii) Kuendelea na ujenzi wa jengo la Utawala Kampasi Kuu Mzumbe;
 - (ix) Kujenga miundombinu ya barabara, umeme, maji safi na majitaka Kampasi Kuu Mzumbe;
 - (x) Kujenga mtambo wa kuchomea taka hatarishi katika Kituo cha Afya Kampasi Kuu Mzumbe;
 - (xi) Kuboresha mfumo wa uhasibu wa kompyuta (Sage ERP ACCPAC);
 - (xii) Kuboresha maabara za kompyuta Kampasi Kuu Mzumbe;
 - (xiii) Kuanzisha maabara ya kompyuta katika Kituo cha Mwanza;
 - (xiv) Kuboresha Mfumo na usambazaji wa

- maji Kampasi Kuu Mzumbe;
- (xv) Kuendeleza eneo la Tegeta Kampasi ya Dar es Salaam;
 - (xvi) Kugharimia mafunzo ya watumishi 36 ambapo 18 katika ngazi ya shahada ya umahiri na 18 katika ngazi ya shahada ya uzamivu; na
 - (xvii) Kuchapisha vitabu kumi na moja (11), makala za kufundishia nane (8) na makala nyingine 59.

Chuo Kikuu Huria cha Tanzania

137. **Mheshimiwa Spika**, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kilianzishwa kwa sheria ya Bunge Na. 17 ya mwaka 1992. Sheria hiyo ilianza kutumika rasmi kufuatia tangazo katika Gazeti la Serikali Na. 55 la mwezi Machi, 1993. Hata hivyo, kufuatia uanzishwaji wa Sheria ya Vyuo Vikuu Na. 7 ya mwaka 2005, Chuo kwa sasa kinaendeshwa kwa kutumia Hati Idhini yake ya mwaka 2007.
138. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2017/18, shughuli mbalimbali zimepangwa kutekelezwa na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania kama ifuatavyo:
 - (i) Kudahili jumla ya wanafunzi 11,100 wa fani mbalimbali ambapo 1000 watadahiliwa ngazi ya Cheti, 1500 watadahiliwa ngazi ya stashahada, 7500 watadahiliwa kwenye Shahada

ya kwanza, 1,000 watadahiliwa shahada ya Uzamili na 100 watadahili shahada ya Uzamivu;

- (ii) Kufanya utafiti katika maeneo ya Mazingira, TEHAMA, Nishati, Kilimo na Chakula, Uongozi na Biashara, Maendeleo ya Utalii, Sheria, Uthibiti wa Ubora, Utawala na Maendeleo, Watu wenye Ulemavu na Mahitaji Maalumu, Maliasili, Umaskini, Utamaduni, Haki za Binadamu, Maendeleo ya Watu na Mawasiliano;
- (iii) Kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu katika nyanja za Mazingira, TEHAMA, Nishati, Kilimo na Chakula, Uongozi na Biashara, Maendeleo ya Utalii, Sheria, Uthibiti wa Ubora, Utawala na Maendeleo, Watu wenye Ulemavu na Mahitaji Maalumu, Maliasili, Umaskini, Utamaduni, Haki za Binadamu, Maendeleo ya Watu na Mawasiliano;
- (iv) Kujenga Maabara ya Sayansi, hosteli za Wanafunzi na Vyumba vyta Madarasa Makao Makuu Bungo, Kibaha;
- (v) Kujenga ofisi za Wafanyakazi, ukumbi wa Mihadhara na vyumba vyta Maabara ya kompyuta katika vituo vyta Mikoa ya Dodoma, Kigoma, Mwanza, Lindi na Manyara;

- (vi) Kukarabati vituo vya Mikoa vya Morogoro (Awamu ya II), Songwe, Kilimanjaro, Lindi, Zanzibar na Simiyu pamoja na Vituo vya Uratibu vya Chato, Kibondo, Kasulu, Nachingwea na Serengeti;
- (vii) Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi na wanafunzi kwa ajili ya kuongeza ujuzi na matumizi ya TEHAMA hasa katika ‘Learning Management System’;
- (viii) Kuweka kozi zote kwenye mfumo wa mtandao (Moodle) ili kurahisisha kujifunza na ufundishaji;
- (ix) Kununua samani kwa ajili ya vituo vya Mwanza, Songwe, na Geita na vifaa vya ofisi; na
- (x) Kufuatilia kwa ukaribu upatikanaji wa hati Miliki za viwanja vya Chuo katika Mikoa mbalimbali na kujenga uzio kwenye viwanja ambavyo havina uzio.

Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili

139. **Mheshimiwa Spika**, Chuo kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi (MUHAS) ni muendelezo wa kilichokuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Afya (MUCHS) ambacho kilianzishwa kwa Sheria ya Bunge, Sheria Na. 9 ya 1991, wakati kitivo cha tiba cha Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam kilipobadilishwa na kuwa Chuo Kikuu

Kishiriki. Mnamo mwaka 2007, MUCHS ilibadilishwa na kuwa MUHAS (Article 1 of the Charter of Incorporation).

140. **Mheshimiwa Spika**, Malengo ya Chuo kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi kwenye Bajeti kwa Mwaka 2017/18 ni kama ifuatavyo;
- (i) Kudahili wanafunzi 1,370 wakiwemo wa Stashahada 340; wa Shahada ya Kwanza 660; wa Uzamili 360 na wa Uzamivu 10;
 - (ii) Kufanya tafiti mbalimbali zikiwemo tafiti za:-
 - Magonjwa yanayoambukiza (infectious diseases) yakiwemo UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu;
 - Magonjwa yasioambukiza (non-communicable diseases) yakiwemo Kisukari, magonjwa ya moyo, ugonjwa wa selimundu (Sickle cell disease);
 - Afya ya uzazi na watoto;
 - Magonjwa yasiyopewa kipaumbele (neglected tropical diseases); na
 - Tafiti za mfumo wa afya nchini (health system);
 - (iii) Kuendelea kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusiana na afya za binadamu;

- (iv) Kuendelea kutoa huduma kwa wagonjwa katika Hospitali ya Taifa ya Rufaa, Muhimbili. Vilevile wanataaluma wa Chuo watatembelea baadhi ya Mikoa kushiriki katika utoaji huduma kwa jamii;
- (v) Kufanya ukarabati wa hosteli, ofisi, maabara na nyumba za wafanyakazi pamoja, ukarabati wa mfumo wa kusambaza maji chuoni (Muhimbili), uwekaji wa ‘lifti’ kwenye jengo jipya pamoja na ukarabati wa uwanja wa michezo;
- (vi) Kuanza Ujenzi wa majengo ya kufundishia, mabweni, maabara na nyumba za wafanyakazi wa hospitali –Kampasi ya Mloganzila;
- (vii) Kuanza Ujenzi wa Kituo Mahiri cha Magonjwa ya Moyo na Mishipa ya Damu;
- (viii) Kuongeza na kuboresha miundombinu ya mawasiliano (ICT infrastructure) pamoja na elimu katika nyanja hiyo kwa wanafanyakazi; na
- (ix) Kuajiri wafanyakazi kwenye maeneo yenye upungufu na kuwaongezea elimu;

Chuo Kikuu Ardhi

- 141. Mheshimiwa Spika,** Chuo Kikuu Ardhi kilianzishwa tarehe 31/9/2008 kutokana na Sheria ya Vyuo Vikuu ya mwaka 2005 (Universities Act, 2005) na baada ya kukidhi kanuni za usajili wa vyuo (TCU, Chartering Registration and Accreditation Procedures Regulation, 2006) pamoja na Hati Idhini ya mwaka 2007 (Ardhi University Charter 2007).
- 142. Mheshimiwa Spika,** Katika mwaka wa fedha 2017/18 Chuo Kikuu Ardhi kinatarajia kutekeleza yafuatayo:
- (i) Kudahili wanafunzi 4,622 katika fani mbalimbali, kati yao wanafunzi 4,372 ni wa Shahada ya kwanza na 250 ni wa Stashahada za Juu, Uzamili na Uzamivu;
 - (ii) Kufanya tafiti mpya kumi na nne (14) katika maeneo mbalimbali yahusuyo ujenzi, usimamizi wa mazingira na matumizi bora ya ardhi. Chuo pia kitaendelea kufanya tafiti thelathi (30) zilizokwishaanza;
 - (iii) Kutoa machapisho 200 yanayotokana na tafiti mbalimbali katika majarida ya nchini na nje ya nchi;
 - (iv) Kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za ujenzi, usimamizi wa mazingira na matumizi bora ya ardhi kwenye miradi nane (8). Chuo pia

- kitatoa huduma kwa jamii kupitia ‘public outreach programs’ tano (5);
- (v) Kukarabati majengo yafuatayo: (a) hosteli za wanafunzi awamu ya IX (b) madarasa, (c) karakana ya useremala, (d) tanki la kuhifadhi maji la ujazo wa lita 600,000, (e) jengo la uchapishaji, (f) nyumba za wafanyakazi na (g) barabara na maegesho ya magari;
- (vi) Kuhuisha mitaala ya mafunzo na kuandaa mitaala mipya (curicula review);
- (vii) Kugharamia mafunzo ya wafanyakazi katika shahada za uzamivu 45, uzamili 54, shahada ya kwanza 12 na diploma na cheti 20;
- (viii) Kukamilisha ujenzi wa jengo la madarasa na ofisi la ‘Lands Building’ awamu ya tano;
- (ix) Kujenga hosteli za wanafunzi 2000 awamu ya I;
- (x) Kujenga jengo la maabara (Multipurpose Laboratory);
- (xi) Kujenga miundombinu mipya ya TEHAMA; na
- (xii) Kujenga mfumo wa maji takatatu, kuunganisha majengo pamoja na kujenga mfumo wa umeme wa juu katika majengo yaliyoko kwenye matumizi.

Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Saalam (DUCE)

- 143. Mheshimiwa Spika**, Chuo Kikuu Kishiriki Cha Elimu Dar es salaam kilianzishwa kupitia tangazo la Serikali Na. 202 lililochapishwa tarehe 22 Julai 2005 chini ya kifungu 55(1) cha Sheria Na. 12 ya mwaka 1970 ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Chuo Kilipewa Hati idhini (Charter) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2010.
- 144. Mheshimiwa Spika**, Malengo ya DUCE katika Mwaka wa Fedha 2017/2018 ni kama ifuatavyo:
- (i) Kudahili jumla ya wanafunzi 2,000 kati yao 700 wa fani ya sayansi;
 - (ii) Ujenzi wa kituo cha utafiti;
 - (iii) Kuimarisha miundombinu ya TEHAMA na kukarabati miundombinu ya umeme;
 - (iv) Kupata ardhi nyingine kubwa zaidi kwa ajili ya upanuzi wa Chuo na pia kufanya upanuzi wa maabara za sayansi, vyumba vyaya madarasa (Awamu ya II) na mfumo mku wa maji taka. Kukarabati majengo na miundombinu ya Chuo;
 - (v) Kuendelea kushirikiana na Vyuo na Taasisi za ndani na nje ya nchi katika utafiti na mafunzo, hususani kwa shahada za uzamili na uzamivu;

- (vi) Kununua vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ajili ya wanafunzi wenyewe mahitaji maalum na Kununua vifaa vya maabara pamoja na madawa (chemicals); na
- (vii) Kuajiri jumla ya wafanyakazi 178 kati yao walimu 75 na waendeshaji 103.

Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere

- 145. **Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA) kilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Namba 6 ya mwaka 2005.
- 146. **Mheshimiwa Spika**, Malengo ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2017/18 ni kama ifuatavyo:
 - (i) Kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka 5,173 mwaka wa fedha 2016/2017 mpaka kufikia 5,900 kwa mwaka wa fedha 2017/2018 na pia kuanza kutoa mafunzo ngazi ya uzamili kwa kuanzia na programu angalau mbili katika Kampasi ya Kivukoni Dar es Salaam.
 - (ii) Kuimarisha miundo na uendeshaji wa idara ya Tafiti na Machapisho na kuimarisha kitengo cha udhibiti ubora ili kuweza kuboresha Elimu inayotolewa kwa kuweka kitengo kwa kila idara na kuboresha mitaala ili

- iweze kwenda na wakati;
- (iii) Kutoa, elimu, usimamizi wa fedha, utunzaji wa kumbukumbu kwa sekta binafsi na sekta ya umma; na
- (iv) kukarabati miundombinu ya chuo hasa madarasa, nyumba za wafanyakazi na ununuzi wa samani;

Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya

147. Mheshimiwa Spika, Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (Mbeya University of Science and Technology - MUST) kilianzishwa mwaka 2012 chini ya Sheria ya Vyuo Vikuu Namba 7 ya mwaka 2005 baada ya kupandishwa hadhi na Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU) kwa iliyokuwa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya. MUST ilitunukiwa Hati Idhini ya Chuo Kikuu (Mbeya University of Science and Technology Charter 2013) mnamo tarehe 20 Agosti 2013.

148. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/18 Chuo kitatekeleza yafuatayo:

- (i) kuongeza udahili wa wanafunzi kutoka wanafunzi 3,982 kwa mwaka wa masomo 2016/2017 hadi kufikia wanafunzi 4,300 kwa mwaka wa masomo 2017/2018,
- (ii) Kuandaa na kukarabati miundombinu ya Chuo katika Kampasi ya Rukwa

- kwa ajili ya kuanza kutoa mafunzo katika ngazi ya stashahada (Ordinary Diploma) kwa mwaka wa masomo 2017/2018; na pia kuendelea na kukamilisha ujenzi wa jengo la Maktaba ili kukidhi mahitaji ya huduma bora za maktaba kwa wanafunzi na wahadhiri;
- (iii) Kuandaa mpango kabambe wa upanuzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya ili kuwa na miundombinu stahiki kwa maendeleo ya Chuo Kikuu; pamoja na kufanya ukarabati wa miundombinu chakavu ya maji, umeme na majengo ya Chuo Kikuu;
 - (iv) Kufanya tathimini ya mali za wananchi waishio katika eneo la hekta 511 la Chuo Kikuu ili kupisha shughuli za upanuzi wa Chuo Kikuu;
 - (v) Kuongeza eneo la Kampasi ya Rukwa kutoka hekta 48 hadi kufikia hekta 500 ili kuwezesha upanuzi wa shughuli za Kampasi hapo baadaye; Kufanya upembuzi yakinifu kwa ajili ya kuanza ujezi wa Ndaki ya Uhandisi na Teknolojia (College of Engineering and Technology);
 - (vi) Kuanza ujenzi wa kituo cha Atamizi za Teknolojia (Technology Incubation Centre) kwa lengo la kuchochaea na kuongeza ubunifu wa teknolojia mpya

- kwa maendeleo ya jamii;
- (vii) Kuanza kutoa mafunzo ya ualimu wa sayansi na mafunzo ya sayansi na teknolojia ya maabara katika ngazi ya shahada ya kwanza ili kuongeza upatikanaji wa walimu wa masomo ya sayansi katika shule za sekondari na vyuo vya ufundu nchini; na
- (viii) Kukamilisha uandaaji wa mitaala mipyä ya kufundishia katika ngazi ya stashahada, shahada kwanza, stashahada ya uzamili, shahada ya uzamili na shahada ya uzamivu.

Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela – NM-AIST

149. Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela Arusha (The Nelson Mandela African Institute of Science and Techology in Arusha-NM-AIST Arusha) ilianzishwa mwaka 2009 chini ya Sheria ya Vyuo Vikuu Namba 7 ya mwaka 2005. Taasisi hii ina jukumu la kutoa elimu na mafunzo katika ngazi ya uzamili na uzamivu pamoja na kufanya utafiti katika ngazi ya ubobezi. Malengo ya Taasisi kwa kipindi kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kuongeza Udhili wa wanafunzi kutoka 213 hadi 350 kufikia Juni 2018;

- (ii) Kufanya mapitio ya mitaala na programu za mafunzo kufikia Juni 2018; pamoja na kusambaza maarifa na kubadilishana mitaala/programu za mafunzo kufikia Juni 2018;
- (iii) Kufanya Utafiti na uchambuzi yakinifu kwa ajili ya Kampasi ya Tengeru kufikia juni 2018;
- (iv) Kuandaa Mpango Mkuu wa matumizi ya ardhi Kampasi ya Tengeru kufanyika kufikia Juni, 2018;
- (v) Kubuni michoro na ujenzi wa jukwaa, vyoo na barabara kwa ajili ya viwanja cha michezo na mfumo wa maji safi kwa vyanzo vipyta vya maji;
- (vi) kubuni na kujenga mfumo wa uondoaji maji taka, kujenga mabweni ya Wanafunzi, kujenga majengo ya ofisi kampasi ya Tengeru kwa ajili ya wafanyakazi 200, vyumba vya madarasa 10 na kumbi 6 ya mikutano pamoja na kubuni na kujenga Kituo cha Afya kufikia Juni, 2018; na
- (vii) Kuanzisha maabara maalum kwa kununua vifaa vya sayansi ya miamba kufikia Juni, 2018 na kufanya ununuuzi wa kompyuta mpakato 9 ifikapo Juni, 2018.

Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam

150. **Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT) kilianzishwa kwa Sheria ua Bunge Na.6 ya mwaka 1997. Taasisi ina jukumu la kutoa mafunzo katika ngazi ya ufundu sanifu na uhandisi; kufanya utafiti na kutoa ushauri wa kitaalamu katika nyanja za Ufundu, Teknolojia na Uhandisi;
151. **Mheshimiwa Spika**, Taasisi hii ina malengo yafuatayo katika mwaka wa fedha 2017/2018.
- (i) Kudahili wanafunzi wapya 1,500 na kuendelea kuhudumia wanafunzi 2,926 wanaoendelea hivyo kuwa na jumla ya wanafunzi 4,426;
 - (ii) Kufanya mapitio ya programu za Stashahada, Shahada na Shahada ya Uzamili pamoja na Kuanzisha kozi mpya za Stashahada ya Uhandisi katika Ujenzi na Barabara; Shahada ya Uhandisi katika Madini; na Shahada ya Uzamili ya Uhandisi katika Nishati Endelevu;
 - (iii) Kuanzisha kozi ya stashahada ya utengenezaji viatu na kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi na ya kitaalamu katika teknolojia ya ngozi kwa lengo la kuongeza thamani ya zao la ngozi kwa wafugaji;
 - (iv) Kukamilisha ujenzi wa jengo la DIT

Teaching Tower awamu ya pili na ya mwisho; na

- (v) Kutekeleza miradi 30 ya huduma za ushauri wa kitaalamu kwa jamii na Kutekeleza mradi wa TELMS awamu ya pili unaofadhiliwa na Serikali ya Italia.

Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi

152. **Mheshimiwa Spika**, Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, kilipata Hati Idhini tarehe 23 Februari, 2015 baada ya kutimiza vigezo vya TCU vya kuwa Chuo Kikuu kamili. Chuo hiki kilianza kama Koleji ya Ushirika mwaka 1963 na baadaye kuwa Chuo Kikuu Kishiriki cha Ushirika chini ya Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kuanzia 2004 hadi tarehe 4 Septemba 2014. Hiki ni Chuo pekee nchini kilichobobea katika kuandaa wataalamu wa Elimu ya Ushirika na fani zinazoshabihiana na ushirika.
153. **Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2017/2018 Chuo kimepanga kutekeleza malengo yafuatayo:
- (i) Kusajili wanafunzi 4,000 kwa mwaka wa masomo 2017/2018 na Kuendeleza mafunzo ya wafanyakazi 70, hususani Wahadhiri katika ngazi za Uzamili na Uzamivu;
 - (ii) Kujenga maktaba yenye uwezo wa kuchukua wasomaji 2500 kwa wakati mmoja;

- (iii) Kukarabati miundombinu ya zamani; kumbi za miadhara, madarasa, mabweni, barabara za ndani, majengo ya ofisi, mfumo wa mawasiliano wa ndani na nyumba za makazi; na
- (iv) Kuendelea kutoa na kueneza elimu ya ushirika nje ya Chuo ili kuchochaea ari ya maendeleo katika jamii kwa kushirikiana na wadau wengine, hususani Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi; Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO); Shirikisho wa Vyama vya Ushirika Tanzania (TFC) na vyama vya ushirika nchini na katika nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa

154. **Mheshimiwa Spika**, Chuo Kikuu Kishiriki Cha Elimu Mkwawa kilianzishwa kupitia tangazo la Serikali Na. 202 la tarehe 22 Julai 2005 chini ya Kifungu 55(1) cha Sheria Na. 12 ya mwaka 1970 ya Chuo Kikuu cha Dar es salaam. Chuo Kilipewa Hati Idhini na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwaka 2010. Chuo hiki kimejikita kuandaa waalimu wa shahada ya kwanza wa sayansi na sayansi za jamii kwa lengo la kuhudumia shule za sekondari nchini.
155. **Mheshimiwa Spika**, Malengo ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa katika

mwaka 2017/18 ni pamoja na:

- (i) Kuboresha ufundishaji wa kiugunduzi na kutumia teknolojia katika ufundishaji katika programu zote za elimu kwa kuunga mkono matumizi ya teknolojia katika ufundishaji na ujifunzaji na ufundishaji wa kiugunduzi, kuongeza udahili wa wanafunzi na kuanzisha Maktaba ya kisasa;
- (ii) Kutoa mafunzo ya kina katika programu za elimu katika ngazi zote kuanzia elimu ya awali, ngazi ya kati mpaka ngazi ya juu ya kada ya ualimu kwamba Taasisi itarekebisha na kuboresha mitaala katika program za elimu na kutekeleza utafiti na uzinduzi wa programu ya elimu ya mazoezi na sayansi ya michezo (PESS);
- (iii) Kuboresha na kutoa mafunzo anuai katika programu za kitaaluma na kiweledi katika nyanja tofauti tofauti kwa kuanzisha programu 3 mpya za shahada ya kwanza, shahada ya umahili na programu mpya za astashahada na stashahada ya uzamili;
- (iv) Kuimarisha uwezo wa Rasilimali watu katika utendaji na utoaji huduma kwa jamii kwa kuimarisha kitengo cha masomo ya uzamili, utafiti

na huduma kwa jamii, kuongeza matokeo yanayotokana na utafiti na ubunifu kutoka machapisho 50 hadi machapisho 250, kukuza na kujenga ushirikiano na mahusiano ya umma;

- (v) Kutangaza Programu za mafunzo yanayotolewa na Chuo kwa kuimarisha Uongozi, Usimamizi na Utawala bora, kuhamasisha na kusimamia ipasavyo rasilimali na fedha za Chuo katika kuimarisha programu za elimu zinazotolewa na Taasisi; na
- (vi) Kuboresha na kuimarisha vitendea kazi na miundombinu ya kufundishia na ujifunzaji kwa kumalizia ujenzi wa ukumbi wa miadhara, ujenzi wa maabara 2 za sayansi, ujenzi wa ofisi na ukarabati wa miundo mbinu ya chuo, uwekaji wa umeme wa jua na uchimbaji wa visima vya maji safi.

Tume ya Taifa ya UNESCO

- 156. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Taifa ya UNESCO ni chombo kinachosimamia utekelezaji wa programu za UNESCO nchini. Jukumu lake kuu ni kuratibu utekelezaji wa Progamu za UNESCO nchini katika Nyanja zake tano ambazo ni Elimu, Sayansi Asilia, Sayansi Jamii, Utamaduni na Mawasiliano na Habari.
- 157. **Mheshimiwa Spika**, Kazi zilizopangwa katika kipindi cha mwaka wa fedha

2017/18 ni kama ifuatavyo:

- (i) Kuratibu utekelezaji wa sheria/miongozo ya UNESCO nchini ikiwa na pamoja na ushiriki wa Tume ya Taifa ya UNESCO katika mikutano ya UNESCO, kuratibu utekelezaji wa programu mbalimbali za UNESCO na pia kuratibu/kutekeleza miradi (participation program) kwa kadri inavyowezekana;
- (ii) Kutaarifu wadau na Kuratibu ufadhili wa UNESCO kimasomo pamoja na Kuitangaza Tume ya Taifa ya UNESCO kupitia vyombo vyahabari;
- (iii) Kushiriki katika kuadhimisha siku 5 za UNESCO na Serikali pamoja na kushirikiana na wadau mbalimbali kisekta;
- (iv) Ufutiliaji wa jarida toleo la 13 la Tanzania na UNESCO na kuandaa jarida toleo la 14 la Tanzania na UNESCO;
- (v) Kuandika mawazo ya miradi (angalau miradi 5) kwa UNESCO na wadau wengine ili kunufaisha Taifa letu;
- (vi) Kuandaa Mikutano kwa ajili ya kuwajengea uwezo vijana ili kuendana na shughuli za UNESCO lakini pia na kumudu kasi ya Malengo ya Dunia Endelevu na kufanya Mkutano na wadau wote ili kuboresha mahusiano;

na

- (vii) Kuanzisha mahusiano na Tume za Taifa za nchi zilizopo katika kanda za Mashariki ya kati ya Afrika.

Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC)

158. **Mheshimiwa Spika**, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TAEC) imeundwa kwa sheria ya Bunge Na. 7 ya mwaka 2003 (The Atomic Energy Act No. 7 of 2003). Majukumu ya Tume ni kusimamia na kudhibiti matumizi salama ya vyanzo vya mionzi, kuhamasisha matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia na kuishauri Serikali juu ya utekelezaji wa mikataba ya kimataifa kuhusu teknolojia hiyo;
159. **Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2017/2018, Tume itatekeleza mambo yafuatayo:
- (i) Kupokea na kutathmini maombi 500 ya leseni mbalimbali ili kuona kama yanakidhi matakwa ya sheria na kanuni za usalama na kinga ya mionzi ya mwaka 2004;
 - (ii) Kuendelea na ukaguzi wa migodi 6 mikubwa inayofanya kazi na migodi mingine itakayobainika, ili kubaini hali ya usalama inayoendelea katika migodi hiyo; pamoja na kuendelea kukagua vituo vyenye vyanzo vya mionzi vipatavyo 150 ili kubaini hali

ya usalama wa wafanyakazi na jamii inayovizunguka;

- (iii) Kusajili vyanzo vya mionzi vipatavyo 1,045 ili kuvitambua na kuhifadhi mabaki ya mionzi yasileté madhara katika mazingira na viumbe hai;
- (iv) Kuendelea na upimaji wa viwango vya mionzi katika sampuli angalau 4,000 za vyakula na mbolea pamoja na kuendelea na upimaji wa viwango vya mionzi (Personnel Dosimetry Service) kwa Wafanyakazi 1,600;
- (v) Kukusanya, kusafirisha na kuhifadhi mabaki ya vyanzo vya mionzi yasiyotumika kutoka vituo vinne na kuyahifadhi katika jengo maalumu (Central Radioactive Waste Management Facility- CRWMF) lililopo Arusha;
- (vi) Kuendelea kuendesha kituo cha kupima mionzi katika hewa ya anga (Radionuclide Monitoring Station-TZP-RN64) kilichopo katika kampasi kuu ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam) chini ya mkataba wa kimataifa wa Comprehensive Nuclear Test-Ban Treaty of Nuclear Weapons (CTBT);
- (vii) Kuendelea kuratibu miradi mipyä sita (6) ya kitaifa, na miradi ya kikanda (AFRA) itakayoanza mwaka

- wa fedha 2017/18 na miradi ambayo bado inaendelea na utekelezaji kwa mwaka wa fedha 2016/17 ambayo inagharamiwa na Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki Duniani (International Atomic Energy Agency-IAEA); na
- (viii) Kufungua vituo vya Kanda ya Kati katika Mkoa wa Dodoma na Kanda ya Nyanda za Juu katika Mkoa wa Mbeya.

Kituo cha Maendeleo DAKAWA

160. **Mheshimiwa Spika**, Kituo cha Maendeleo Dakawa kina majukumu ya Kutunza na Kuhifadhi majengo, vifaa, na miundombinu yote iliyokabidhiwa na ANC kwa ajili ya kulinda historia ya Ukombozi wa Afrika Kusini. Mipango ya Wizara ni pamoja na kukiendeleza kituo na kukitumia katika kutoa Elimu ya Sayansi, TEHAMA na Ufundi.
161. **Mheshimiwa Spika**, Kazizitakazotekelzwa katika mwaka 2017/18 ni kama ifuatavyo:
- (i) Kuhakikisha kuwa Mazingira ya Kituo yamehifadhiwa na kubaki kama ilivyokuwa enzi za ANC;
 - (ii) Kuendelea kufuatilia Hati Miliki ya Kituo kilichokabidhiwa na Serikali toka ANC ya Afrika Kusini; na
 - (iii) Kuendelea kufuatilia Uandaaji wa

Muundo wa Kisheria wa Uendeshaji wa Kituo.

Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA)

162. Mheshimiwa Spika, Katika mwaka 2017/18, Mamlaka ya Elimu Tanzania imepanga kutoa ufadhili katika Taasisi na maeneo yafuatayo;

- (i) Ujenzi wa nyumba nane (8) za walimu katika Shule za Sekondari zilizopo kwenye mazingira magumu na maeneo yasiyofikika kwa urahisi;
- (ii) Ujenzi wa vyoo 50 katika shule zenyne upungufu mkubwa wa vyoo baada ya kufanya tathmini;
- (iii) Kutoa mikopo ya elimu kwa Taasisi za Elimu 10 kwa ajili ya kuwezesha ujenzi wa miundombinu na ununuzi wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia;
- (iv) Ujenzi na uimarishaji wa miundombinu ya elimu kwa wanafunzi wenyenye mahitaji maalumu katika Taasisi 20 za Elimu na Mafunzo; na
- (v) Kuendelea na ukarabati kwa Shule Kongwe za Sekondari za Serikali nchini; na kuendelea na ujenzi wa mabweni ya wanafunzi wa kike katika Shule za Sekondari kwenye mazingira magumu na maeneo yasiyofikika kwa urahisi.

D. SHUKRANI

163. **Mheshimiwa Spika**, Napenda kutambua mchango mkubwa wa Viongozi wenzangu katika kufanikisha majukumu ya Wizara yangu. Kipekee kabisa namshukuru sana Mheshimiwa Mhandisi Stella Martin Manyanya (Mb) Naibu Waziri kwa ushirikiano mkubwa anaonipa. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Dkt Leonard Douglas Akwilapo; Manaibu Makatibu Wakuu; Profesa Simon Samwel Msanjila na Dkt. Ave Maria Semakafu, Kamishna wa Elimu, Wakurugenzi, Wakuu wa Vitengo na Wakuu wa Taasisi mbalimbali zilizo chini ya Wizara yangu kwa ushirikiano wao wa karibu katika kutekeleza majukumu ya kila siku ya Wizara yetu. Pia namshukuru Bi. Maimuna Kibenga Tarishi aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara yangu hadi alipohamishiwa kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu (Bunge).
164. Napenda pia kuwashukuru, Viongozi wa Vyama vya Wafanyakazi, Watumishi wa Wizara, Wanataaluma, Wanafunzi na wadau wote wa Elimu kwa ushirikiano wao katika kuendeleza Elimu, Sayansi na Teknolojia. Ninatambua na kuthamini sana mchango wenu mzuri katika kuhakikisha kuwa sekta ya elimu nchini inaendelea kuimarika.

165. **Mheshimiwa Spika**, Napenda kuwashukuru wadau wote wa Sekta ya Elimu, Sayansi na Teknolojia wakiwemo Washirika wa Maendeleo, Viongozi mbalimbali na wananchi wote ambao wamechangia sana katika kufanikisha utekelezaji wa Mipango ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.
166. **Mheshimiwa Spika**, Washirika mbalimbali wa Maendeleo na wadau wa Elimu wamechangia katika kufanikisha Mipango ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Kwa kuwa si rahisi kuwataja wote, napenda kuchukua fursa hii kwa niaba ya Wizara yangu, kuwashukuru na kuwatambua baadhi yao kama ifuatavyo: Serikali ya Algeria, Canada, China, Cuba, India, Italia, Japan, Urusi, Denmark, Finland, Norway, Marekani, Mauritius, Msumbiji, Misri, Sweden, Uingereza, Ujerumani, Korea Kusini, Uturuki, Ubelgiji na Jumuiya ya Afrika Mashariki.
